jasiriamali Mtafutaji

ISSN No: 0856 - 9843

Toleo Na. 02 Juni 2005

Jarida la wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati

Mtafutaji agombaniwa Dar

Umaskini ni mzigo uliotulemea ?

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

DAI pesa private enterprise support activities

DAI PESA PROJECT is a USAID funded

Mtafutaji mag2.indd 1

6/28/05 2:43:07 PM

Quality Printers

Colour Print Tanzania's aim is to keep in step with all of our clients requirements.

Your work will be monitored through our Client Care procedures throughout its production, this process will continue until you receive the completed project on your doorstep.

The after care will then commence, we will keep a check on the quality of our service to you, continually updating our records on all of the work that we carry out for you, making every effort to perform all tasks efficiently and keep you informed along the way.

"communication is everything"

COLOUR PRINT TANZANIA LIMITED

50-Nelson Mandela Expressway, P.O.Box 76006, Dar es Salaam, Tanzania.
Telephone: (+255-22) 2450331 / 2450845 / 2450802 Fax: (+255-22) 2450332
Email: info@colourprintz.com
Website: www.colourprint-tz.com

Mtafutaji mag2.indd 2 6/28/05 2:43:28 PM

yaliyomo

Mtafutaji
Juni 2005 Vol. 2

	Ukurasa
Tuukatae Umaskini	4
Ujasiriamali ni suluhisho	5
Umuhimu wa masoko ya mazao ya wakulima wadogo	7
Halima Rashidi na Uwezeshaji wa Wanawake	10
Wakulima wa Ruvuma wanufaika na VICOBA	12
Umaskini ni Mzigo uliotulemea?	13
DAI PESA watoa mafunzo ya kilimo Hai/UKIMWI	16
Mbinga Kurugenzi Saccos wanufaika	17
Mikopo kama silaha ya kupambana na umaskini	17
Waathirika wa UKIMWI watumiwa kama kitega uchumi	18
Vikundi vya Wakulima vyaunda shirikisho	19
Masharti ya mikopo yawaathiri wakulima wadogo wa miwa	21
Chama cha Ushirika kuanzisha Sekondari	21
Somo la Biashara na familia	22
Mjue Ra P	23
Tatizo la ajira kwa vijana	24
Ufafanuzi wa sheria ya uandikishaji Mashirika	25
Shirika la Pride Tanzania lakopesha Wafanyakazi	26
Burke ahimiza wakulima kuunda vikundi	26
Vijue vikundi vya akina mama wa Temeke	27
SACCOS za wanawake Ruvuma zakopeshwa mifugo	29
Wadau wataka marufuku ya Lumbesa itekelezwe	29
Iringa Vijijini kuuaga umaskini?	30
Ruvuma wafunzwa kilimo cha Pilipili mboga	31
Uzalishaji miwa kupanda	31
Viongozi wa shirikisho watembelea Moshi	32
RUMACU SACCOS ya jengewa uwezo	32
Washauriwa kutafuta masoko kwa komputa	33
Teknolojia yetu itumike kupambana na Umaskini	34
Utafiti wa Mazingira	35

Linatayarishwa na kusambazwa
na
Opportunities Industrilization Centres of Tanzania
(OIC Tanzania)
S.L.P. 12474,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: (255) 22-2775705,
Faks: (255) 22- 27772734
Simu ya Kiganja: +255-744 276018
Baruapepe:mtafutaji@gmail.com

Bodi ya Wahariri
Mr. Kawa Kundaeli- Mwenyekiti
Mr. E.B. Tonya - Mhariri Mkuu - 0744 989785
Mr. Canute W. Temu - Mwakilishi DAI PESA
0748 320 690/ 0744 282 101
Mrs. Halima Rashid - Mhariri Msaidizi
-0748596899

Design & Layout
ColourPrint (T) Ltd

Kama tulivyoona katika toleo lililopita la Mtafutaji, tunaendelea kukuletea mada mbali mbali ambazo ukizisoma, ukizingatia na ukizitendea kazi zitakusaidia kuwa mjasiriamali hivyo utaukataa umaskini.

Kama jina la jarida lenyewe lilivyo, MTAFUTAJI, basi ni wajibu wa kila mmoja wetu kutamani kuwa mtafutaji na mbunifu, na si kukaa tu na kusuburi kwamba serikali itakuja kutukwamua kutoka kwenye umaskini. Sisi wenyewe tujishughulishe na tutafute ni wapi pana fursa ya kuweza kufanya kazi yoyote iliyo halali ili kujipatia kipato badala ya kukaa tu na kuilaumu serikali.

Nia yetu hasa ni kutaka kuwashauri na kuwaelekeza wananchi jinsi wanavyoweza kuondokana na umaskini, kwa mfano:

- Kukubali kwamba wewe mwenyewe waweza kuutokomeza umaskini ulio nao
- Kuwa wajasiri na kutafuta ni wapi penye fursa ya kuweza kuendesha biashara au kilimo.
- Kutafuta ni wapi wanaweza kupata mtaji au mikopo na kuifanyia biashara.

Wengi wetu tunafahamu kwamba adui yetu mkubwa ni umaskini ambao pamoja na maradhi na ujinga ni maadui watatu wa mwanadamu. Tunaweza kuwatokomeza maadui hawa wote kama tukiukataa umaskini.

Umaskini umekuwa ukipigwa vita tangu enzi na enzi kwa kuelezewa kwenye vitabu na magazeti na pia kwa maneno, bila mafanikio makubwa. Sasa ni wakati wetu kuupiga vita umaskini kwa vitendo kwa kuuchukia na kuukataa tukiamini kwamba sisi hatukuzaliwa tuwe maskini bali tumekuwa maskini kwa sababu ya kutokuzitumia fursa zilizopo na zinazojitokeza vizuri. Ni jukumu la kila mmoja kuacha uvivu na kusimama katika nafasi yake mwenyewe ili kuutokomeza umaskini, badala ya kuachia serikali na viongozi wetu mzigo huu. Wengi wa viongozi wetu wa kisiasa na hata walio serikalini siyo wajasiriamali hivyo hata dhana ya ujasiriamali ni ngeni kwao. Laiti kama viongozi wangalijengewa uwezo wa kuelewa ujasiriamali ni nini, ingelisaidia sana kwani wangeupiga vita umaskini kwa nguvu zao zote kuliko sasa ambapo maneno ni mengi kuliko vitendo.

Ipo hadithi ya wananchi waliobetweka baada ya kuona kwamba kila walipopungukiwa chakula serikali yao ilikuwa ikiwapelekea chakula cha msaada, ingawaje eneo waliloishi lilikuwa zuri, lenye mvua za kutosha na ardhi yenye rutuba sawa na mabonde ya milima Usangu na ile ya Kilimanjaro. Wananchi hawa walikuwa wakulima hodari na wazalishaji wazuri wa chakula, lakini wakabweteka baada tuu ya nchi yao kupata uhuru. Siku moja Raisi wao alipokuwa njiani kwenda kuzuru eneo hilo, alikutana na msafara wa malori ulioshеheni nafaka ukielekea huko. Akauliza kulikoni? Akaambiwa wenyeji wa eneo hilo wananjaa na wasipopata msaada haraka watakufa. Inasemekana aliamuru malori hayo yarudi yalikotoka. Alipowahutubia wananchi wa eneo lile aliwaeleza wazi wazi kwamba ameamuru chakula kilichokuwa kikiletwa huko kirudishwe kilikotoka ili wananchi wale wajifunze. Aliendelea kuuliza kwa mshangao inawezekanaje eneo lililokuwa likitoa chakula cha kutosha na hata ziada ya kuuza nje ya nchi yao kabla ya Uhuru, leo hii waletewe misaada ya chakula wakati upo ushahidi kwamba mvua zilikuwepo za kutosha na zilinyesha kwa wakati. Aliwaonya wananchi wale kwamba liwalo na liwe hawataletewa chakula, ni bora wachache wafe njaa ili liwe fundisho la kuwaponya wananchi wengine.

Hakuna mwenye uhakika kama wapo waliokufa, lakini cha kujifunza hapa ni kwamba kwa zaidi ya miaka 40 sasa wananchi wa eneo lile hawajapata kuwa na upungufu wa chakula. Kwa muda wote huu, wamekuwa wakizalisha zaidi ya mahitaji yao.

Watanzania tulio wengi hatutofautiani na wananchi walioelezwa katika mfano huu. Tumebweteka, tunapenda kutoa majibu rahisi kwamba sasa tufanyeje; hatuna mitaji na vitendea kazi. Hivi wengine wanapata wapi mitaji? Wao wameanzishaje miradi yao?

Kutoka Kwa Mkurugenzi Mtendaji

"TUUKATAE UMASKINI"

Hatuna malengo, na mara nyingi hata wachache tunao kutana nao kwenye mafunzo au kwa ushauri, huishia kulalamika tuu bila kuwa na uhakika wa kitu mtu alichopanga kufanya. Hivi kama hujapanga unachotaka kufanya, au kama huna hata wazo la biashara ukiupata huo mtaji utaufanyia nini? Wengi wameshuhudia kwenye mafunzo yaliyopita ya ujasiriamali hivi karibuni kwamba, walidhani wakipata mitaji watafanya tuu biashara bila matatizo. Walipopata mikopo waliishia kuitumia kwa mambo tofauti kabisa na biashara. Hivi sasa wanapata adha kubwa ya kuirudisha mikopo hiyo kwa vile hawana biashara na fedha walishazitumia.

Ushauri wetu kwa wasomaji kama itakavyoonekana katika mada mbalimbali zilizoandikwa kwenye jarida hili, ni muhimu kwa watu kuamua kubadilika sasa na kuwa watafutaji wenye malengo na wanaoamini kwamba wataweza. Kwa sasa ni wakati muafaka kwa Watanzania kuachana na mawazo potofu kwamba hatuwezi kuuondoa umaskini. Ni muhimu sana kubadilika kimawazo kwani tusemapo hatuwezi na akili zetu nazo hukubali hatuwezi hivyo, tukishaamini hivyo tunakuwa hatuwezi asilani.

Jarida hili litaendelea kuhubiri juu ya kuukataa umaskini, na badala yake tuamini kwamba tuano uwezo wa kuzalisha utajiri (ability to create wealth).

Mtafutaji mag2.indd 4 6/28/05 2:43:38 PM

Toka Meza ya Mhariri

UJASIRIAMALI NI SULUHISHO

Wapendwa wasomaji,

Awali ya yote kumradhi, kwani toleo hili la jarida mlipendalo limechelewa kuingia mitaani. Pamoja na wingi wa sababu zinazoeleweka kuwa "nje ya uwezo wetu", ukiwemo ucheleweshaji wa rasimu za makala na habari, bado makataa yote ni yetu. Hata hivyo maulizo yenu ya daima yameufunua upenzi wenu wa MTAFUTAJI na pia nia yenu njema ya kushiriki katika kuliendeleza jarida hili.

Katika toleo la kwanza tulielimishana kuhusu dhamira ya jarida letu hili na mantiki nzima ya ujasiriamali katika kupambana kuundoa umaskini. Na tunaendelea kufanya hivyo katika toleo hili na yajayo. Hebu sasa tushirikiane katika kuungalia UJASIRIAMALI kama suluhisho la matatizo yanayotusibu sisi wanadamu katika maisha yetu. Kwa ufupi tunauongolea ujasiriamali kama nyenzo muhimu katika juhudi zetu za kujijengea UWEZO WA KIUCHUMI ili tuweze kuwa na hali bora zaidi na hadhi katika jamii kama watu wengine. Tukiwa na uwezo wa kiuchumi tutaweza kujipatia huduma muhimu katika maisha yetu. Muhimu zaidi, tutaweza kuundoa unyonge na kushiriki katika michakato ya kisiasa na kijamii kwa kujiamini.

Kwa leo tuliangalie tatizo la AJIRA MBAYA YA WATOTO na jinsi linavyoweza kutatuliwa kupitia ujasiriamali, yaani kwa kufanya shughuli za kibiashara pamoja na kilimo kitaalamu zaidi; kwa kuwa wawekezi wenye mipango bora.

Matokeo ya tafiti mbalimbali, ukiwamo ule ambao OICT tulishiriki mwaka 2003/2004, yanaonyesha kwamba sababu kuu ya ajira mbaya ya watoto ni UMASKINI uliokithiri katika kaya. Umaskini wa kipato hujinyumbua katika nyanja nyingine za umaskini, k.m. ukosefu wa uhakika wa chakula, watu kushindwa kuzimudu huduma muhimu kama elimu ya watoto na afya, makazi duni, kushindwa kuzitumia vyema maliasili kama misitu na samaki ambayo huharibiwa, kushindwa kuwa na sauti katika jamii au kushiriki katika mipango, ufuatiliaji na maamuzi na kubakia wanyonge. Laiti kama tungalitumia mbinu za kijasiriamali, ambazo zinafafanuliwa katika makala karibu zote zilizomo katika toleo hili, tungekuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kumudu maisha, tena kwa kujiamini.

Takwimu za Taifa zinaonyesha kwamba kwa wastani Mtanzania wa kawaida anaishi kwa kutumia chini ya dola moja ya Kimarekani kwa siku, labda kwa kutumia shilingi mia tano, sijui.
Hali hiyo huwakosesha elimu na huduma nyingine watoto wa familia. Na ikiendelea hivyo, watoto hao nao pia watashindwa kumudu kuzitegemeza familia zao, na hivyo mzingo huo wa umaskini utaendelea. MUNGU APISHIE MBALI! Watoto wengi waliokosa fursa ya kwenda shule huingia katika ajira ambazo haziendani na umri wao na huwaathiri vibaya kimaumbile, kisaikolojia, kiafya na huwadhalilisha. Aina za ajira hizo ni pamoja na kuchuuza vitu mitaani, upakazi, kuzoa taka kwa mikokoteni, kuvunja mawe/ kugonga kokoto, kilimo katika mashamba ya mabepari k.m. ya tumbaku, kazi za majumbani ambako wengi wao hudhalilishwa sana, kazi za migodini ambako wanatumiwa kama "nyoka" wa kuingia ndani ya mashimo hatari kabisa na pia kuchekecha mchanga, kuuza vileo katika mabaa na vilabu vya kienyeji, kuhudumia katika nyumba za wageni, kuchunga mifugo ya watu wengine, na ukahaba wa kulazimishwa.

Mtafutaji mag2.indd 5
6/28/05 2:43:43 PM

Katika ajira zote hizo, pamoja na ubaya uliopo, waajiriwa wanadhulumiwa kimapato. Tumewahi kuhojiana na wauza baa ambao walituarifu kwamba walikuwa wanalipwa mshahara wa shilingi elfu nane hadi kumi kwa mwezi. Hao ni watu wenye watoto, wanapanga vyumba na inawabidi wajikimu kimaisha. Kwa vyovyote hawana budi kuwa na njia nyingine halali za kujiongezea kipato. Lakini ni siri iliyo wazi kwamba baadhi yao hujiingiza katika biashara zisizokuwa rasmi wala halali, kama ukahaba. Na ukahaba huu unaweza "kurithishwa" pia, k.m. mama mlea peke anapokuwa kilabuni na "wateja" wake wasipomkuta nyumbani, basi kibinti chake kinachokutwa hapo hulazimishwa "kuchukua zamu" (rejea matokeo ya Majadiliano ya Vikundi Lengwa katika Uchambuzi wa Hali Halisi ya Ajira Ya Watoto 2003). Ukahaba au biashara ya ngono imeongezewa kasi na kuporomoka kwa maadili ya jamii kufuatia ujaji wa maendeleo ya teknolojia k.m. televisheni na intaneti, pia na matokeo ya utandawazi. Ujenzi wa mahoteli ya ufukweni nao umetoa mwanya kwa watu wasiopenda shughuli halali "kujimwaga" katika biashara ya ngono, tena ngono zenyewe za hovyo hovyo, pamoja na ushoga, ngono kinywa na ngono mwaranda. Amri za Mungu za MLIMANI namba 6 na 9 zimedharauliwa kabisa! Eti wanasema "uhuru wa binadamu"!? Haya kwa Mwenyezi kwa kuwa na shingo ngumu na kuuchafua mwili safi na roho pia. Hatimaye wanafamilia na majirani wanateseka kwa kuwalea wagonjwa na kukosa huduma. Ripoti ya Umoja wa Mataifa inaeleza kwamba mwaka huu 2005 kumetokea vifo vingi zaidi vinavyotokana na UKIMWI kuliko kabla. Na kati ya watu milioni

Wanafunzi wakirudi toka likizo: Je tuna watayarisha vipi watoto wetu wasiingie katika ajira mbaya?

40 wenye UKIMWI duniani, idadi kubwa wapo katika nchi zetu zinazoendelea ambako asilimia 12 tu ya wagonjwa wanaweza kupata dawa za ARV.

ni matumizi mabaya ya sera za utandawazi.

Mada yetu si ukahaba au biashara ya ngono, la hasha; bali tunataka tuyaone madhara ya kuzembea kufanya shughuli kijasiriamali ili tujitegemee kiuchumi na tuzikoe familia zetu. Madhara ya biashara ya ukahaba yapo wazi: ni maradhi ya kaswende ya muda mrefu na UKIMWI, iwapo hatutaji dhambi

Watoto wetu wataangamia na Taifa litaangamia tusipoongeza juhudi za kiuchumi kwa kutumia mbinu za kijasiriamali, ili watoto wasiingie katika biashara au ajira haramu.

Kuna miradi mingi ya kuwaelimisha na kuwakopesha akina mama wafanyabiashara wadogo. Haina maana kwamba akina baba ndio wanatakiwa waangamie, hapana. Ni kweli kwamba ukimwelimisha mwanamke wa Kiafrika umeielimisha na umeiokoa kaya. Aidha, tafiti zilizotajwa hapo juu zilionyesha kwamba wazazi/walezi wengi wa watoto waliokutwa kwenye ajira mbaya walikuwa akina MAMA WALEA PEKE. Lakini jambo la muhimu zaidi ni kwamba mapato ya biashara aifanyayo mama yanaifaidia familia nzima, pamoja na baba na kaka.

Iwapo tunabuni miradi yenye mipango na tunaitekeleza kijasiriamali, familia zetu zitashikamana, watoto watasoma na hawataingia katika ajira mbaya. Mbinu za kijasiriamali ni pamoja na kuunganisha nguvu zetu wafanyabiashara, pamoja na wakulima, katika vikundi na mashirikisho. Tuachane na woga na tudiriki kufanya kazi kibiashara lakini tuwe makini, tukizingatia ushauri wa kitaalamu unaotolewa na wabia wa maendeleo yetu wakiwemo OIC Tanzania na DAI PESA.

Mtafutaji mag2.indd 6 6/28/05 2:43:48 PM

Umuhimu wa masoko ya mazao ya wakulima wadogo

Na Abel Lyimo: Mshauri wa Vikundi na Sera katika mradi wa DAI PESA unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Kimarekani (USAID).

Utangulizi

Kilimo ni mojawapo kati ya sekta muhimu katika kuuinua uchumi wa Tanzania. Mnamo mwaka 2003 kilimo kilichangia asilimia 51 ya fedha za kigeni. Asilimia 80 ya ajira zinapatikana kwenye kilimo na asilimia 46.8 ya pato la taifa inatokana na kilimo. Kwa sababu hii maendeleo ya kiuchumi ya Tanzania hayawezi kupatikana kama sekta ya kilimo ni dhaifu. Pamoja na nafasi hii muhimu ya kilimo nchini, wananchi waishio vijijini bado ni maskini wakubwa wa kipato. Sababu kubwa ya umaskini huo ni ukosefu wa masoko mazuri na ya uhakika ya mazao ya wakulima wadogo.

Nchi ambazo zimefanikiwa kupunguza umaskini kati ya wananchi wake ni zile ambazo zimetatua kero ya masoko za wakulima wake. Upatikanaji wa masoko mazuri ni kichocheo cha mabadiliko mengine ya kiuchumi, kwa mfano:-

1) Upatikanaji wa ajira,
2) Uanzishaji viwanda vidogo,
3) Ongezeko la watoa huduma kama wauza pembejeo, n.k,
4) Kuongezeka kwa huduma za usafirishaji,
5) Ongezeko la matumizi ya mafuta ya kuendeshea magari na mitambo mingine,
6) Ongezeko la wigo wa kutoza ushuru kuanzia ngazi ya kijiji hadi serikali kuu
7) Kupanuka kwa biashara nyingine kama za migahawa,

Jee uzalishaji unazingatia mahitaji ya soko?

baa, mama ntilie, n.k.,

8) Ongezeko la shule za binafsi,
9) Upatikanaji wa sadaka na zaka – kwa ajili ya kuwahudumia walemavu, waishio na VVU/UKIMWI, watoto wa mtaani na watu wengine wenye shida,
10) Uboreshaji wa lishe.

Ukosefu wa masoko ya uhakika una athari mbaya, kwa mfano :-

i) Ukosefu wa ajira – uzururaji, ulevi na matokeo yake yakiwemo vitendo vya kifisadi,
ii) Kushindwa kutengeneza miundo mbinu,
iii) Kushindwa kusomesha watoto,
iv) Kushindwa kuendeleza ardhi.

Kuna madhara mengi sana yanayotokana na kutokuwa na uhakika wa masoko ya mazao yanayolimwa na wakulima. Kimsingi umaskini hautapungua iwapo kuna ukosefu wa masoko yenye manufaa.

Mtafutaji mag2.indd 7 6/28/05 2:43:51 PM

1. Mfumo wa soko huru

Upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa ajili ya mazao ya wakulima katika nchi zinazoendelea utawawezesha wakulima kushiriki moja kwa moja katika kuongeza uchumi na hivyo ukuaji wa kuchangia pato la taifa. Kwa sasa hivi mchango wa wakulima wadogo mmoja mmoja katika kuongeza pato la taifa ni mdogo sana.

Kama wakulima hawashiriki katika kuongeza pato la taifa basi madhara niliyoyataja hapo juu yatadhihiri, hali ambayo imeanza kujitokeza nchini Tanzania. Utafutaji wa masoko mazuri kwa ajili ya wakulima ni muhimu zaidi katika nchi maskini kuliko katika nchi zilizoendelea.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Ushirika na Masoko, tangu soko huru lianze mwishoni mwa miaka ya themanini biashara ya mazao ya kilimo inafanywa na wafanyabiashara wachache na uwekezaji ni mdogo sana. Mawasiliano kati ya wakulima na wanunuzi wa mazao yao ni hafifu na kuna uhaba wa miundo mbinu, hasa vijijini. Taarifa hiyo, inaongeza kwamba maghala hayatumiki inavyostahili na kuna ukosefu mkubwa wa mtaji kwa wakulima wadogo.
Aidha, imedhihirika kwamba wakulima wengi hawajanufaika na mfumo wa soko huru kwa sababu hawajajipanga. Vyama vingi vya ushirika vimeshindwa kushindana na wanunuzi binafsi sababu havikuandaliwa vizuri. Utandawazi unaozungumzwa kwenye vyombo mbalimbali haujaeleweka vizuri kwa wakulima. Ni wakulima wachache wanaoamini kwamba wanaweza kuuza mazao yao nje ya nchi.

Tafiti mbalimbali zimeonyesha kwamba kuanzia ngazi ya uzalishaji hadi uuzaji tija ni ndogo sana hapa Tanzania. Hali hii inasababisha bei ya mazao katika soko la nje kuwa kubwa kiasi kwamba mazao hayo hayawezi kushindana katika soko la kimataifa. Pia pato la mkulima hupungua kutokana na gharama kubwa za uzalishaji.

2. UKIMWI na soko huru

Soko huru limechangia ongezeko la kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi. Wafanyabiashara toka sehemu mbalimbali ndani na hata nje ya nchi hufuata mazao vijijini. Mara kwa mara wanajadili bei na mkulima mmoja mmoja na wanaweza kumaliza mwezi wakiwa vijijini, hasa msimu wa mavuno. Kwa vile wanakaa muda mrefu vijijini na wanakwenda huko mara kwa mara, ni rahisi kushiriki vitendo vya ngono na wenyeji ambavyo husababisha kuenea kwa maambukizo ya ukimwi; kwa misingi kwamba asilimia 70 ya wakulima wa vyakula vijijini ni wanawake, wakati zaidi ya asilimia themanini ya wanunuzi wa mazao ya wakulima ni wanaume.

3. Mikataba ya mauzo

Kukosekana kwa vikundi/vyama vilivyosajiliwa kisheria kumewafanya wakulima wadogo wengi washindwe kufunga mikataba ya kisheria ya mauzo. Baadhi ya wafanyabiashara wanatumia hila ili walipe bei ndogo kwa mazao ya wakulima wadogo. Wanawakopesha pesa wakulima wakati wana shida na kuwasainisha mikataba ya kununua mazao yao yatakapokomaa. Kwa vile

wakulima
hao hawajaungana wanakosa nguvu ya kisheria ya kuchukua hatua zozote wanapogundua kwamba wamesaini mikataba ambayo inawakandamiza kwa kulipwa malipo kidogo sana kwa mazao yao. Aidha wakulima wanashindwa kuingia kwenye kilimo cha mikataba kwa sababu ya ukosefu wa elimu ya biashara.

4. Ukosefu wa elimu ya biashara na masoko

Wakulima wadogo wamezoea kulima kiasili na ni wazito kwenda na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia. Mabadiliko makubwa yanayokwenda kwa kasi kubwa, hasa uendeshaji biashara katika mfumo wa soko huru, yamewaacha wakulima wadogo kwenye mataa. Ukosefu wa elimu sahihi ya biashara na masoko kwa wakulima wadogo umewafanya wakulima hao washindwe kuendesha kilimo chao kibiashara na kwa faida. Aidha wafanyabiashara wengi hawana elimu ya biashara na masoko katika mfumo wa soko huru. Mapungufu haya kwa pande zote mbili, wakulima na wafanyabiashara, yamesababisha kupanda kwa gharama za masoko na uzalishaji.

5. Upatikanaji wa pembejeo

Mfumo wa soko huru uliwaruhusu wanunuzi binafsi kuingiza pembejeo toka nje ya nchi na kuzisambaza kwa wakulima nchini. Ingawa pembejeo zinapatikana nchini, wakulima wengi wanashindwa kuzipata kutokana na kutokuwepo kwa chombo cha kuwasaidia kupata mikopo.

Idadi kubwa ya vyama vya ushirika ambavyo vingewatafutia wanachama wake mikopo ya pembejeo, vilishindwa kufanya hivyo kutokana na kutokukubalika na vyombo vya fedha. Hali hii imechangia kushuka kwa tija katika uzalishaji wa mazao. Nao ubovu wa barabara toka mijini kwenda vijijini umechangia kupanda kwa bei ya pembejeo na pia pembejeo hizo kuchelewa kuwafikia wakulima.

6. Muhtasari wa matatizo ya masoko

i) Ukosefu wa masoko mazuri na ya uhakika,
ii) Ukosefu wa taarifa za bei katika masoko,
iii) Ukosefu wa mtaji,
iv) Ukosefu wa magulio,
v) Ukosefu wa elimu ya biashara,
vi) Ukosefu wa mizani na utumiaji wa vipimo visivyoku wa sahihi,
vii) Ufahamu mdogo wa kilimo cha mkataba,
viii) Gharama kubwa za uzalishaji na usafirishaji,
ix) Kutokuwa na sera za masoko zinazoeleweka na wakulima.

Biashara ya inahitaji uelewa wa soko

7. Ushauri

i) Uundaji na uimarishaji wa vikundi vya wakulima/vyama vya ushirika ili viwe na nguvu ya kujadili bei na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi kwa niaba ya wakulima,
ii) Uanzishaji wa magulio ya kuaminika,
iii) Utumiaji wa vipimo sahihi vya mazao,
iv) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo,
v) Upatikanaji wa dawa sahihi za kuhifadhia nafaka na utumiaji wa ghala ili kuyauza mazao baadaye wakati bei ziko juu.

8. Mwisho

Kwa miaka mingi kilio cha wakulima wadogo kimekuwa ni ukosefu wa masoko ya uhakika. Wataalamu mbalimbali wameandika mada zinazoelezea ufumbuzi wa matatizo ya masoko kwa wakulima wadogo. Hata hivyo, idadi kubwa ya wataalamu hao wanaishi katika maeneo ya mjini, hasa Dar es Salaam na wana uzoefu mdogo wa maisha ya mkulima mdogo anayeishi kijijini. Hivyo wanaandika wakitumia nadharia tete zaidi kuliko uhalisi.

Njia mojawapo inayoweza kuwasaidia wakulima kutatua tatizo la masoko ni wao kuungana na kuuza mazao yao kwa pamoja. Wakulima wakiweza kuunganisha nguvu zao katika chama ni rahisi kwao kupanga bei, kama wanavyofanya wazalishaji wa mafuta wa umoja wa "OPEC". Pia ni rahisi kutafuta masoko mazuri ndani na nje, kwani wanunuzi hupendelea kununua mazao mengi yaliyo mahali pamoja, kuliko yaliyosambaa kidogo kidogo katika sehemu tofauti.

Wakulima wanaweza kukusanya mazao yao kwenye ghala la chama na kuyauza baadaye wakati bei ziko juu. Aidha asasi zinazotoa mikopo zinapendelea zaidi kutoa mikopo kwa wakulima waliojipanga na kuunda muungano unaoeleweka na wenye nguvu. Kwa njia hizo wakulima wataweza kupata maisha bora zaidi siku za baadaye.

Abel Lyimo ataendelea na mada zake katika matoleo yajayo.
MHARIRI

HALIMA RASHIDI NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE

Mnamo mwezi Julai mwaka 2003 OIC-Tanzania ikishirikiana na mfuko wa McKnight wa huko Amerika ilianzisha mradi wa majaribio wa mwaka mmoja wa kuwaendeleza akina mama wafanyabiashara ndogo ndogo, wakiwemo wakulima wa bustani za mboga, mama lishe, watengenezaji wa batiki na "tie & die". Kwa kifupi mradi huu unaitwa "WEP" (yaani Women's Economic Empowerment Programme").

Kwa makusudi kabisa mradi huu uliwalenga akina mama wa wilaya ya Temeke, wanaoishi katika kata za Kurasini na Mivinjeni kwa sababu Temeke ndiyo iliyo nyuma zaidi kimaendeleo ikilinganishwa na wilaya nyingine mbili za Dar es Salaam, yaani Kinondoni na Ilala.

Mradi huu umeweza kuwafikia akina mama zaidi ya 750 katika muda huu wa majaribio, ambao wamepata mafunzo ya ujasiriamali na hatimaye wamepata mikopo toka WEP ili waweze kuendesha biashara zao kijasiriamali. Mradi huu una vikundi 75 vya watu kati ya 10 - 15. Wanawake hawa hupewa mikopo kwa masharti ya kujidhamini wao wenyewe katika vikundi vyao. Kutokana na mafunzo ya ujasiriamali wanayoyapata, akinamama hawa wameweza kurejesha mikopo kwa asilimia 100. Sasa wanamudu kujikimu wao wenyewe na familia zao kimaisha. Wanawake hao sasa wanafanya biashara zao kwa kujiamini na mafanikio makubwa zaidi.

Pamoja na mazuri yote haya, yapo pia matatizo katika urejeshaji wa mikopo. Kama ambavyo inavyojulikana, mama ndiye nguzo ya familia na mara nyingi huelemewa na mzigo mzito wa kuitunza familia. Matokeo yake ni kwamba baadhi yao wanajikuta wanatumia pesa za mkopo kuhudumia familia na hivyo kufanya biashara ambayo hailingani na pesa walizopewa. Hali hii husababisha ugumu na usumbufu katika urejeshaji wa mkopo. Baada ya kushauriwa na kuelimishwa zaidi, tatizo hili limekoma.

Wapo pia akina baba ambao wakijua wake zao wana mikopo, basi hata pesa za chakula nyumbani hawatoi tena. Hali hii inaleta utata katika biashara. Shime akina baba, waacheni wake zenu wafanye biashara kwanza ndipo watumie sehemu ya faida kwa matumizi ya nyumbani. Wasaidieni na wapeni moyo ili waweze kupanua biashara zao kwa manufaa ya familia.
Haya, akina mama wenzangu, tujifunge vibwebwe tufanye biashara. Tuachane na tamaa za kuvaa kila nguo inayotoka dukani eti ili "niende na wakati". Wakati gani? Tafuta kwanza! Tumelala kwa karne nyingi, sasa tujitahidi alaa kulihali tuupate usawa katika jamii zetu kwa kuwa na nguvu za kiuchumi. Nanyi waume, halahala na ushauri wangu, wasaidieni wake zenu wajiendeleze na mikopo ya WEP ili familia zenu zipate ahueni ya maisha!

Sikilizeni kikundi cha akina mama kilivyoufurahia mkopo wa WEP na ni hao ndio waliopata ushirikiano wa waume zao,
Nanukuu: " Mradi huu wa WEP umekuwa na manufaa sana kwetu, tunaiomba OICT iweze kuupanua ili tuweze kuendelea kunufaika na hata uwafikie akina mama wenzetu wa sehemu nyingine", alisema mmoja wa wanakikundi.

Halima Rashid ni Mratibu wa Mradi wa OIC Tanzania wa kuwaendeleza kiuchumi wanawake (WEP). Halima pia ni mkufunzi wa ujasiriamali. Ndiye alitupambia gazeti akisimamia usambazaji wa Mtafutaji

Mtafutaji mag2.indd 10 6/28/05 2:43:58 PM

SHIRIKA LA MASOKO YA KARIAKOO

Baadhi ya mazao yaliyopokelewa sokoni Kariakoo kuanzia tarehe 11 hadi 17 June 2005

Zao	Mkoa linakotoka	Soko la jumla			Soko la rejareja		
		Kipimo uwingi	Bei		Kipimo	Bei	
			Chini	juu		Chini	Juu
Karoti	Arusha, Nairobi*	Gunia 660	35000	50000	Kg	500	800
Njegere mbichi	Iringa	Gunia 2315	10000	25000	Kg	400	1000
Kabichi nyeupe	Arusha, Tanga, Iringa	Lumbesa 504	25000	40000	@	200	600
Nyanya maji	Iringa	Tenga 6219	10000	20000	Kg	300	600
Vitunguu maji	Manyara, Singida	Lumbesa 1327	30000	45000	Kg	300	500
Mboga za majani	Morogoro, Pwani, DSM, Dodoma	Mfuko 830	7000	16000	Fungu	30	100
Machungwa	Tanga, Morogoro, Pwani	@ 229000	9	30	@	20	80
Embe mbivu	Mombasa	Kasha 56	10000	25000	@	150	400
Matikiti maji	Arusha	@ 4992	300	1200	@	350	1500
Ubuyu	Dodoma	Mfuko 51	8000	12000	Kg	400	500
Matunda damu	Tanga	Tenga	-	-	Kg	-	-
Apple (matofaa)	Iringa, Tanga	Tenga	-	-	Kg	-	-
Ndizi mbivu	Tanga, Morogoro, Pwani	Tenga 1473	5000	30000	Chane	150	1470
Ndizi mbichi	Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro	Mkungu 645	2400	15000	Fungu (4-5)	200	1500
Viazi mviringo	Iringa, Tanga, Kilimanjaro	Lumbesa 3941	25000	35000	Kg	250	350
Viazi vitamu	Morogoro	Mfuko 5	30000	34000	Fungu	200	1000
Magimbi	Morogoro	Mfuko 15	16000	17000	Fungu	200	500
Muhogo	Pwani, DSM	Mfuko kosovo 106	9000	35000	Fungu	150	300
Njugu nyasa	Dodoma, Malawi	Lumbesa 23	60000	90000	Kg	500	1000
soya	Iringa	Gunia -	-	-	Kg	700	1000
Choroko	Dodoma	Gunia 144	40000	50000	Kg	600	800
Kunde	Dodoma	Gunia -	-	-	Kg	500	700
Maharagwe	Iringa	Gunia 3	60000	-	Kg	650	800
Nazi	Mombasa, Pwani, Tanga,	Gunia 4635	19000	22000	@	110	250
Vitunguu saumu	Mbeya	Lumbesa 1	-	96000	Kg	1000	1400
Tangawizi	Kilimanjaro	Lumbesa 6	48000	60000	Kg	600	800
Hiliki	Morogoro	Gunia -	-	-	Kg	2500	3000
Abdala yasini	Morogoro	Gunia 2	-	28000	Kg	1000	1500
Dagaa	Rukwa, Kigoma	Gunia 122	125000	180000	Kg	2800	4000
Pilipili Mboga	Iringa, Kilimanjaro	Mfuko 289	28000	42000	kg	500	800

Mtafutaji mag2.indd 11 6/28/05 2:44:03 PM

WAKULIMA WA RUVUMA WANUFAIKA NA "VICOBA"

Na Assumpta Mwamtende, ambaye ni Afisa Mtendaji katika mfumo wa "Village Community Banking (VICOBA)" Songea

VICOBA" ni mfumo wa kuweka na kukopa ambao unatumiwa na wakulima wa vijiji vilivyo katika Kata ya Mletele, Wilayani Songea. Mfumo huu sasa unaenezwa katika vijiji vya sehemu nyingine kadhaa za mkoa wa Ruvuma, nje ya wilaya ya Songea.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mfumo huo Mkurugenzi Mtendaji wa VICOBA, Mheshimiwa Diwani Devota Likokola alielezea kilichomsukuma kuuasisi mfumo huo. Wakulima wa vijiji hivyo hawakuwa na namna yoyote ya kuzihifadhi fedha zao ili ziweze kuongezeka nao kupata fursa ya uwezo mkubwa zaidi kifedha na kulima kama wajasiriamali. Matokeo yake ni kwamba walibaki maskini na yumkini wangeendelea kuwa hivyo kwa muda usiojulikana.

Mheshimiwa Devota Likokola, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Songea, alifanya utafiti wa kina na kuyabaini matatizo ya wakulima hao. Ndipo alitokeza na ufumbuzi wa kuanzisha "VICOBA", mahsusi kwa ajili ya kuweka na kukopa vijijini, tarehe 1 Machi, 2004.

Mfumo wa VICOBA unaendeshwa kwa kutumia vikundi. Imani za kidini, asili ya mtu atokako au jinsia si vigezo katika uundaji wa vikundi hivi. Kila mwenye sifa za kutosha anakaribishwa kujiunga na kikundi kwa hiari yake mwenyewe. Katika kata ya Mletele peke yake kuna vikundi 20 vya VICOBA na wanachama wake wameelezea viwango vya juu vya kunufaika na mfumo huu.

Katika juhudi zake za kuuboresha mfumo huu ili uwezo wa VICOBA na wakulima uongezeke na matokeo ya VICOBA yaliyotarajiwa yaweze kupatikana, Mh. Likokola amewahi kuwaalika wageni mbalimbali ili watoe ushauri wao. Kutokana na kubadilishana uzoefu, wakulima waliongeza juhudi na sasa wanalima kwa ufanisi zaidi mazao ya maharage, alizeti, kunde miti na pilipili mboga au hohoa (paprika). Ili kuwapa hamasa zaidi wakulima hao, Mheshimiwa Likokola amejitahidi daima kuwatafutia wakulima hao masoko kwa ajili ya mazao yao. Aidha, wakulima wanawezeshwa kwa kupewa mbegu. Kwa ajili ya msimu huu zimeletwa kilo 5200 za mbegu za maharage kupitia VICOBA, zenye thamani ya shilingi 5,460,000.00.

Baada ya kuyaona mafanikio hayo wakazi wa mkoa wa Ruvuma wamehamasika na wanajiunga kwa wingi katika vikundi vya VICOBA. Wananchi wengi wameomba vikundi hivi vienezwe katika maeneo yao na tayari vimeundwa vikundi vipya katika maeneo ya Namtumbo (vikundi vitano) na Wilayani Tunduru (vikundi vitano).

Jambo moja zuri lililojitokeza ni uibukaji wa ujasiriamali. Kabla ya VICOBA wakulima walikuwa "wabangaizaji" tu, wakijilimia chakula chao. Hata mauzo kidogo waliyoyafanya hayakuwa katika mpango wa kimaendeleo kibiashara. Hivyo si ajabu, kwa mfano, waliishiwa kabisa mazao na fedha pia, na daima "walianza upya" kila msimu. Baada ya mfumo wa VICOBA kuingia vijijini, sasa wakulima wanajitahidi kuwa WATAFUTAJI na wanaendesha maisha yao kiujasiriamali.

Mtafutaji mag2.indd 12 6/28/05 2:44:07 PM

UMASKINI NI MZIGO ULIOTULEMEA?

Makala ya Yusuf Makuri, WEP

Katika sehemu nyingi hapa nchini asasi na watu binafsi hutoa mafunzo na mikopo kwa lengo la kupambana na umaskini, lakini matokeo ya juhudi hizo si mazuri kama yalivyotegemewa. Katika hali hii umaskini ambao unaainishwa kuwa ni ukosefu wa uwezo wa kumudu mahitaji muhimu katika maisha, hususan ukosefu wa kipato, chakula, malazi, mavazi na huduma za kijamii, hautaisha.

Takwimu zinaonyesha kwamba Watanzania wengi wanaishi kwa kutegemea matumizi ya dola moja au chini ya hapo kwa siku. Umaskini huu umekithiri zaidi katika maeneo ya vijijini. Tabia ya vijana wengi kuvikimbia vijiji vyao na kwenda kuishi mijini wakitarajia maisha bora nayo inaukithirisha umaskini huo.

Umaskini umeleta athari mbaya nyingi kwa wananchi, kwa mfano ueneaji wa ukahaba, ubakaji, wizi, ujangili na ujahili, uzembe na uzururaji vijiweni n.k. Umaskini umewafanya watu au wasiwe wanajali au watafute njia za mkato ili kujipatia riziki.

Licha ya juhudi za serikali, mashirika ya kifedha na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kupunguza makali ya maisha kwa kutoa mikopo midogo na mafunzo ya namna ya kuitumia mikopo hiyo kwa faida, bado umaskini ndio kwanza unapamba moto. Watanzania tunaonekana kama vile tunauengaenga umaskini, tena kwa hiari yetu wenyewe.



Kuendelea kwa umaskini katika hali hii kunadhihirisha pia kwamba mikopo inayotolewa haitumiwi ilivyokusudiwa. Na kwa sababu hiyo mikopo hiyo hailipwi na mzunguko wa umaskini hauishi.

Hebu tuzipitie sababu chache za wakopaji, hasa wadogo wadogo kutokulipa mikopo, ili tuweze kutafuta ufumbuzi.

- Mikopo mingi hairejeshwi kwa sababu wakopaji ni ndugu, jamaa au marafiki wa maafisa mikopo katika asasi za fedha. Hali hii inazuia ufuatiliaji makini; kwani miiko na taratibu tayari zinakuwa zimekiukwa na kunakuwepo kuoneana haya. Utamuua vipi nyani ukiwa unamwangalia usoni?

- Mikopo hutolewa chini ya mikataba dhaifu (weak contracts) bila ya kuzingatia masuala ya kisheria yatakayombana mkopaji anapolegalega katika matumizi ya mkopo.

- Mikopo mingine hutolewa baada ya wafanyabiashara kuwa wameisotea sana na hata pengine wametoa *mlungula*, ili kuharakisha mambo. Hali kama hii ya kupata mikopo kwa njia za rushwa ni hatari na mara nyingi huvuruga taratibu za utoaji wa mikopo na kusababisha wakopaji wasilipe mikopo kama inavyotakiwa. Wanakuwa wameingia gharama zisizo rasmi ambazo hawana budi kuzirudisha. Hata afisa aliyechukua hongo anakosa ujasiri wa kufuatilia madeni.

- Mikopo mingi ya kiserikali hutolewa kisiasa zaidi kuliko kuangalia mahitaji na malengo halisi ya mkopaji katika kuukuza ujasiriamali. Matokeo yake ni wakopaji kubweteka na kudhani kwamba wamepewa bakshishi na si mkopo unaotakiwa kulipwa kwa muda maalum.

- Sera za serikali kuhusu utoaji mikopo kwa wananchi wa kawaida hazijulikani kwa walengwa; ndiyo maana mara nyingi mikopo ya serikali hutolewa kwa wingi kwa mfano nyakati za chaguzi mbalimbali au vikao vya Bunge, kama kampeni ya zima moto tu badala ya kuwa programu endelevu. Kutolewa kwa mikopo hobelahobela kunaondoa nguvu ya serikali kuwanufaisha wakopaji na kusaidia maendeleo yao. Wakopaji nao hawaoni sababu ya kuwajibika kuilipa mikopo hiyo na wanaweza kuitumia kwa manufaa tofauti na ilivyokusudiwa, kwani aghalabu wanaokopeshwa hawana biashara yoyote au huwa wababaiji tu.

Suala la Mtanzania maskini kujiepua kutoka

Mtafutaji mag2.indd 13 6/28/05 2:44:09 PM

kwenye lindi la umaskini halitegemei kupewa mikopo au mafunzo tu, bali kwanza maskini mwenyewe ajitambue kwamba yu maskini na anahitaji kuchukua hatua za kuundoa umaskini kwa gharama yoyote ile.

Pia anapaswa kutambua kwamba hana budi kutumia nguvu zake mwenyewe ili kujipatia riziki yake na ya familia yake katika ulimwengu wa leo wa utandawazi, ambao umejaa ushindani mkali na wa kikatili.
Ni katika kujitambua huku ndipo maskini ataanza kutafuta mbinu mbalimbali za kuzalisha mali na kutafuta masoko ya kuuzia mazao yake. Pia anaweza kutafuta mkopo na mafunzo ili kuongeza ustadi, nguvu na ujasiri katika uzalishaji mali au uboreshaji wa bidhaa au huduma anazotoa, ili kukidhi mahitaji ya wateja wake na kupata faida.

Mkopaji lazima awe na mpango wa biashara na afanye biashara akiutekeleza mpango huu kwa shuruti, hatua kwa hatua. Atafanikiwa na atamudu kuulipa mkopo. Kazi muhimu ya wakopeshaji itakuwa, pamoja na utoaji wa mikopo, mafunzo na ushauri, kufuatilia kwa karibu mabadiliko ya ukuaji wa shughuli za kibiashara za wakopaji, hata kama wanarejesha mikopo kwa asilimia 100. Na lengo liwe ni marejesho kwa asilimia mia moja.

Ni kwa kufanya hivi ndipo tutaweza kuumudu mzigo wa umaskini, usituzidi nguvu, na tutautua kwa kishindo hautatuelemea.

Jambo muhimu ni kuamua kufanya kazi kwa bidii, maarifa na nidhamu na kupima matokeo ya malengo tuliyojiwekea kila baada ya kipindi maalum. Nina hakika tunao uwezo wa kuutua mzigo wa umaskini tukidhamiria kufanya hivyo.

Kazi kubwa ya serikali itakuwa ni kuandaa mazingira mazuri kwa wananchi kuweza kuzalisha na kuuza mazao, bidhaa au huduma zao bila urasimu wala mizengwe yoyote. Serikali pia iwasaidie na iwalinde wananchi ili waweze kushindana kwa ufanisi katika soko huria linaloingiliwa sasa na wageni.

Mwezeshaji wa OIC Tanzania - WEP akiendesha mafunzo ya ujasiriliamali kwa maafisa wa JWTZ wastaafu.

UFAFANUZI WA MANENO TULIYOYATUMIA, NA MHARIRI MKUU:

ENGAENGA - DEKEZA, ENDEKEZA

LEMA - KUSHINDIKANA, KUWA GUMU.
- TENDEA = LEMEA, TENDEANA = LEMANA
- TENDEKA = LEMEKA, TENDESHA = LEMESHA

MATANGAZO MADOGO MADOGO

Nafasi hii ni kwa ajili ya matangazo madogo madogo ambayo hayatalipiwa

- Matangazo ya Kazi
- Viwanja vinavyouzwa
- Nyumba, makazi
- Mashamba
- Vifaa mbalimbali
- Mifugo
- Magari
- Afya
- Mafunzo
- Mengineyo

Mtafutaji
Barabara ya Samnujoma baada ya FGC Mwenge
Simu Na. 0744 626114, 0744 989785, 0748 276018

Mtafutaji mag2.indd 15 6/28/05 2:44:23 PM

DAI PESA WATOA MAFUNZO YA KILIMO HAI NA UKIMWI

Na Mawazo Malembeka, Iringa.

Wanachama wapatao 440 wa vikundi vya wakulima wamenufaika na mafunzo ya kilimo hai na UKIMWI yaliyotolewa na DAI PESA katika wilaya za Iringa Vijijini na Kilolo hivi karibuni. Mafunzo hayo ni mmoja kati ya mikakati ya DAI PESA (mradi wa kuiendeleza sekta binafsi) ya kukabiliana na tatizo la UKIMWI katika vikundi vya wakulima na ushirika vinavyosaidiwa na Mradi huo pamoja na jamii kwa jumla.

Akiongea na Mtafutaji mkufunzi wa mafunzo hayo ambaye pia ni bibi shamba katika kijiji cha Mangalali, Bi.Sauda Omary alieleza kwamba Kilimo Hai ni kilimo kinachohusisha uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa kutumia mbinu za asili. Bi.Omary alizitaja baadhi ya mbinu hizo kama matumizi ya mboji, matumizi ya samadi na kutumia madawa ya asili kwa ajili ya kuwadhibiti wadudu na magonjwa ya mimea, kutengeneza matuta maalum, kupanda mazao yanayosaidiana kwa nafasi inayofaa na kubadilisha mazao kila msimu wa kilimo.

Bibi shamba huyo alieleza kwamba umuhimu wa mradi huo ni kuwapunguzia gharama wakulima, hususan wakulima wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kupunguza athari zitokanazo na madawa ya viwandani. Chini ya mradi huo, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanashauriwa kulima eneo linaloanzia nusu ekari na wapande mbogamboga na mazao ya chakula ambayo yatawasaidia kuimarisha lishe yao ili waurefushe muda wao wa kuishi, pamoja na kuwahakikishia usalama wa chakula. Bibi Omary aliendelea kueleza kwamba ili juhudi za DAI PESA za kuboresha sekta binafsi hapa nchini zifanikiwe hapana budi kuziunganisha na mapambano dhidi ya UKIMWI. “Hakuna asiyefahamu jinsi tatizo la UKIMWI linavyozidi kukua siku hata siku. Hivyo wenzetu hawa wa DAI PESA wamelitambua hilo na wamelitafutia mbinu ya kupambana nalo na kwa sasa wameanzia kwenye vikundi vinavyosaidiwa na Mradi kwanza,” anasema Bi.Omary.

Alisema kwamba ingawa kilimo hicho kinawalenga moja kwa moja watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wanachama wote wa vikundi wanafundishwa kutokana na ukweli kwamba watu wengi hawajahamasika kiasi cha kutosha kuweza kujitokeza hadharani wanapogundulika kuwa na virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo idadi ya wagonjwa itaongezeka katika muda mfupi ujao.

OPPORTUNITIES INDUSTRIALIZATION CENTERS OF TANZANIA (O I C TANZANIA)

MAONO YA OIC TANZANIA:

Kuongoza katika kuondoa umaskini kwa kuuelimisha umma.

Mtafutaji mag2.indd 16 6/28/05 2:44:28 PM

MBINGA KURUGENZI SACCOS WANUFAIKA

ALBANO MIDELO, SONGEA

Mbinga Kurugenzi SACCOS iliyopo wilaya ya Mbinga, mkoani Ruvuma imewakopesha wanachama wake zaidi ya shilingi milioni 447 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Mwenyekiti wa SACCOS hiyo, Bwana FORKWARD KOMBA aliyekuwa anatoa maelezo ya maendeleo ya chama hicho hivi karibuni Mjini Mbinga, alisema kwamba utoaji wa huduma ya mikopo ya fedha taslimu kwa wanachama wake umekuwa ukiongezeka kila mwaka.

Akifafanua, Bw.Komba alieleza kwamba mwaka 2002 mikopo yenye thamani ya shilingi 75,609,000.00 ilitolewa, mwaka 2003 mikopo yenye thamani ya shilingi 145,572,000.00 ilitolewa na mwaka 2004 thamani ya mikopo ilikuwa ya shilingi 225,902,000.00.

Aidha Bwana Komba alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2003 SACCOS hiyo iliwakopesha wanachama wake vifaa mbalimbali vikiwemo bati, saruji, nondo, mashine za video na jenereta za umeme, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 100,000,000.00. Aliongeza kwamba katika kipindi hicho SACCOS hiyo iliwakopesha wanachama wake mashine za kusaga nafaka 33 zenye thamani ya shilingi 26,940,000.00 na mwezi Januari mwaka huu Mbinga Kurugenzi SACCOS iliwakopesha wanachama wake pikipiki 23 zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 45.

Katika maelezo yake Bwana Komba alisema pia kwamba hadi kufikia Desemba, 2003 wanachama wa SACCOS hiyo walikuwa wamenunua hisa zenye thamani ya shilingi 42,707,000.00 na hadi Desemba 2004 jumla ya hisa zenye thamani ya shilingi 72,707,000.00 zilikuwa zimenunuliwa.

Mbinga Kurugenzi SACCOS ilianzishwa mwaka 1978 kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika ya mwaka 1968 kifungu cha 10 ikiwa na wanachama 51. Hivi sasa SACCOS hiyo ina wanachama 1500.

MIKOPO KAMA SILAHA YA KUPAMBANA NA UMASKINI

Na Halima Rashid, WEP - OICT

Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na asasi za fedha kadhaa hapa nchini ambazo zinatoa mikopo kwa masharti nafuu kuliko mabenki na hivyo kuwasaidia watu wa kipato cha chini kuweza kufaidika na mikopo. Asasi hizo ni pamoja na OICT, PRIDE Tanzania, FINCA, YOSEFO na mengineyo. Mikopo midogo mingi inawalenga wanawake wasio na uwezo kifedha na wafanya biashara ndogondogo ambao hawana dhamana za kuweka benki ili waweze kupata mikopo.

Mashirika haya yanatoa msaada mkubwa katika harakati za kupambana na umaskini. Lakini swali la kujiuliza ni je, mikopo hii kweli husaidia kuondokana na umaskini?

Mikopo ikitumiwa vizuri ni nyenzo muhimu za kuondokana na umaskini. Matumizi mazuri ya mikopo ni yale yanayolenga kutekeleza mipango ya biashara. Lazima mfanyabiashara awe ametengeneza mpango wa biashara yake na ndipo achukue mkopo. Hapa atakuwa anautumia mkopo ili kutekeleza yale ambayo yamo katika mpango wake wa biashara na hivyo biashara itaenda vizuri na kuleta faida, ambayo si tu itasaidia katika matumizi ya familia bali pia itatumika katika kupanua biashara na kujiongezea kipato.

Mtafutaji mag2.indd 17 6/28/05 2:44:30 PM

Watu wengi, hasa akina mama ambao wana mipango mizuri ya biashara wameweza kuitumia fursa hii ya mikopo na kufanya biashara mbalimbali kwa mfano mama lishe, ufugaji wa kuku, kilimo cha mbogamboga, utengenezaji wa nguo za batiki na "tie & dye" na nyinginezo. Kutokana na biashara hizi wameweza kujiongezea kipato na hivyo kuweza kuishi maisha yenye furaha kwani wanaweza kuwapeleka watoto wao shule na hata kulipa gharama za matibabu ya familia bila matatizo makubwa.

Hebu tumwangalie mama huyu na tupate maelezo mafupi kuhusiana na biashara yake.
Mama Kilango alianza biashara ya kutengeneza batiki katika eneo dogo nje kidogo ya nyumba yake. Baada ya kupata mkopo aliamua pamoja na kutengeneza batiki, lakini pia awe na wanafunzi japo wachache ili aweze kuwafundisha na pia wasaidiane katika shughuli za uzalishaji na utengenezaji wa batiki. Hivi sasa mama huyu ana shule ambayo inaweza kuchukua wanafunzi zaidi ya watano kwa wakati mmoja. Mama Kilango alianza kwa kutengeza upya mpango wa biashara. Alikopa pesa katika misingi ya mpango huo, ambao pia ulihusisha kuwafunza ufundi wasichana lakini wakati huo huo wakimsaidia kuongeza uzalishaji. Aliutumia mkopo wake vizuri sana na baada ya mwaka mmoja akawa anazalisha mali maradufu. Hao wasichana baadaye walijiunga naye katika kikundi cha uzalishaji.

Kina mama, hebu tuamke na tutengeneze mipango mizuri ya biashara ili tuweze kuitumia na kupata mikopo ambayo hutolewa na asasi nyingi tu hapa nchini.

Kwa upande mwingine ambao ni kinyume kabisa na mfano wa Mama Kilango, baadhi ya akina mama wamejikuta wakijiingiza kwenye mikopo bila kuwa na mipango mizuri ya biashara. Matokeo yake wanashindwa kuirejesha mikopo hiyo kwani hawana biashara ya uhakika. Badala yake wanazitumia fedha hizo katika mambo tofauti na biashara na kujikuta wanaingia kwenye madeni ambayo yanawazidishia umaskini.

Nawaomba kina mama tujenge tabia ya kuandaa mipango ya biashara ili tuweze kurudisha mikopo na kuendelea kukopa. Kumbuka usemi usemao "Dawa ya deni ni kulipa". Ni kwa kufanya hivyo tu tutaweza kuona matunda ya mikopo katika kuupiga vita umaskini. Vinginevyo tutaendelea kulalamika na hakuna atakayeweza kutusaidia katika kujikwamua na umaskini.

Tuangalie mifano ya wenzetu ambao wamefanikiwa katika biashara zao na tuwe na wivu wa kimaendeleo ili nasi tuweze kufanya biashara na kufanikiwa kama wao.

WAATHIRIKA WA UKIMWI WATUMIWA KAMA KITEGA UCHUMI

Na Iddy Mkwama, Sumbawanga

WANANCHI na wadau mbalimbali wanaoshiriki katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa ukimwi wametakiwa kuacha mara moja tabia ya kuwafanya wagonjwa wa ukimwi kama sinema au kuwatumia kama kitega uchumi cha kujiingizia kipato.
Kauli hiyo imetolewa na mwenyekiti wa chama cha watu wanaoishi na virusi vya ukimwi SHIDEPHA+ Mkoani Rukwa Bw.Godfrey Mwikala alipokuwa akimkaribisha Mbunge wa jimbo la Sumbawanga mjini Mh. Paul Kimiti, alipotembelea ofisi ya chama hicho iliyopo mjini hapa.
Mwikala alisema kuwa kumeibuka tabia kwa baadhi ya wadau ambao wanashiriki katika mapambano dhidi ya gonjwa hatari la ukimwi na wananchi ambao ndugu zao wameathirika, kuwatumia waathirika hao kama njia ya kujipatia kipato. Wadau hao huwachukua waathirika na kuzunguka nao sehemu mbalimbali zenye mkusanyiko wa watu na kuwaonyesha kama sinema. Mara kadhaa watu hao hukusanya pesa kwa madai ya kuwasaidia wagonjwa hao, lakini huzitumia kwa kujinufaisha wao wenyewe na kuwaacha waathirika wakiwa kama kitega uchumi.
"Sisi waathirika wa ukimwi sasa tumenyimwa thamani ndani ya jamii. Tunafanywa kama sinema, tunatembezwa huku na kule kuonyeshwa kwa

Mtafutaji mag2.indd 18 6/28/05 2:44:32 PM

watu na mara nyingine tunatumiwa kufanyiwa harambee, ambapo sasa wametugeuza kama chombo cha kujipatia mapato", alisema Mwikala.
Mwenyekiti huyo aliendelea kusema kwamba wakati sasa umefika kwa wanajamii kuwahurumia wagonjwa wa ukimwi na kuwapa thamani kama watu wengine kwa kuwaweka karibu zaidi na jamii. Aliwataka waathirika na jamii kwa ujumla kutokukubaliana na mtu yeyote ambaye atataka kumtumia ndugu yake ambaye ameathirika kwa madai ya kutaka kumsaidia, kumbe anajiingizia kipato binafsi.

Hata hivyo Mwenyekiti Mwikala alichukua nafasi hiyo kulishukuru shirika la Dai -Pesa kwa kuwapatia msaada wa mara kwa mara na kuwasaidia katika kuishi kwa matumaini.
Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini, Mh. Paul Kimiti, aliwataka wanajamii kujitolea kwa hali na mali kuwasaidia watu wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa ukimwi. Aliwasihi viongozi nchini kulitambua gonjwa hili kama janga linalowagusa watu wote na hivyo washiriki katika kupambana nalo kwa kuwasisitizia wananchi katika sehemu zao kujikinga dhidi ya ukimwi.
"NB: Mimi ni mwandishi wa habari. Nipo mkoani Rukwa na naandikia gazeti la Tanzania Daima. Mwisho. Iddy Mkwama"

VIKUNDI VYA WAKULIMA MOROGORO VYAUNDA SHIRIKISHO

Morogoro ni mkoa unaosifika sana kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na mbogamboga.

Na Sophia Iddi, Morogoro

Hivi karibuni wakulima wa mboga mboga na matunda wa Mkoa wa Morogoro waliweka historia kwa kuunda shirikisho la wakulima wa mboga na matunda la mkoa. Wakulima hao pia walifanya uchaguzi wa viongozi wao. Wafuatao walichaguliwa kuliongoza shirikisho hilo, vikundi vyao wanavyotoka vikiwa katika mabano.

Mwenyekiti: Abdu Matemelela (CHANGA Farmers' Association-Mkuyuni)

Makamu Mwenyekiti: Bi. Venesta Kibua (TWIGHUTZE Farmers' Association-Tchenzema Mgeta).

Katibu: Bi. Janet Mbiki (TWANGE HAMWE Farmers' Association-Langali Mgeta).

Mweka Hazina: Bi. Prisca Dimosso (MTOBOZI Farmers' Association-Matombo)

Wawakilishi wa vikundi 14:

1. Bi. Scholastica Baltazar (CHAWAKABU- Bunduki Mgeta)
2. Ezekiel Changamno (CHAWAKAKI-Kikeo Mgeta)
3. Bi. Edmara Flumenzi (TWIGHUTZE-Tchenzema Mgeta).
4. Benedict Mizambwa (TWANGE HAMWE-Langali Mgeta).
5. Abdallah Ramadhani (Kibwaya Farmers' Association, Mkuyuni)
6. Jumanne Mfaume (Luholole Farmers' Association, Mkuyuni)
7. Mohamed Mzigira (Kungwe Farmers' Association, Mkuyuni)
8. Bi. Farida Ahmed (Kivuma Farmers' Association, Mkuyuni)
9. Hamza Iddi Digonile (Changa farmers'

Mtafutaji mag2.indd 19 6/28/05 2:44:34 PM

Association, Mkuyuni)
10. Rogath Andreas (Gozo Farmers' Association, Matombo)
11. Charles Gendaeka (Nige Farmers' Association, Matombo)
12. Filbert Joachim (Kiswira Farmers' Association, Matombo)
13. Bi. Anna Daudi Mwenda (Tambuu Farmers Association, Matombo)
14. Twaibu Abdu Niga (Mtombozi Farmers' Association, Matombo).

Maelezo ya Mhariri wa Mtafutaji

Tumeichapisha taarifa hii fupi sana kwa kusudio maalum, kwani inayo mafunzo mengi sana kwa wakulima wadogo. Yafuatayo ni baadhi tu ya mafunzo hayo:-

• Uchaguzi wa uongozi huo ulifanywa katika misingi ya demokrasi kwa kutumia kura.

• Uongozi wa kidemokrasi unaotoa fursa kwa wanavikundi wote kushiriki, ni nguzo muhimu sana ya uendelevu wa vikundi kuliko kuwa na uongozi wa kuteuliwa na vyombo vya ngazi za juu na kisha kupachikwa katika vikundi vya wakulima. Huo haupokeleki.

• Shirikisho kama hili lililoundwa Morogoro lina manufaa makubwa kwa wanachama wake na wakulima wanakuwa na nguvu ya kuweza kushindana katika soko huru na pia kuyalinda maslahi yao kisheria, ilimuradi shirikisho hilo lisajiliwe na kitengo husika katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

• Baadhi ya manufaa ya kuwa na mashirikisho ni haya:

(i) Kupata mitaji / mikopo:
- Wakulima wajasiriamali wadogo wanapokuwa na chama kikubwa kinachotambulika na kuendeshwa vyema wanakubaliwa kirahisi zaidi kupata mikopo. Asasi za fedha nyingi ziunakubali umoja wa wanachama kama dhamana ya kupata mikopo.

- Wakulima wadogo waliojiunga katika umoja unaotambulika pia wanaweza kuanzisha chama chao cha kuweka na kukopa (SACCOS) na hivyo kuweza kukopeshana wenyewe ili hatimaye kulitatua tatizo la ukosefu wa mitaji kati yao.

(ii) Kuwa na sauti moja:
- Sauti ya shirikisho ni kubwa na inaweza kuwasilisha ujumbe wa wanachama katika ngazi mbalimbali, pamoja na zile za kitaifa.

(iii) Kupata soko:
- Soko linaweza kupatikana kwa urahisi watu wanapojiunga pamoja na inakuwa rahisi hata kukodi usafiri kwa pamoja kwa ajili ya kusafirisha bidhaa mbali na eneo zinapozalishwa, ili kuweza kupata soko la uhakika na bei ya juu.
(iv) Kujenga ghala la kuhifadhia mazao
- Shirikisho linaweza kabisa na kwa urahisi zaidi kujenga ghala la kuhifadhia mazao na hivyo kuepukana na tatizo la kupata hasara kutokana na mazao kuozea shambani au kuliwa na wanyama waharibifu.

(v) Uwezo wa kupanga bei:
- Shirikisho ambalo limesjiliwa linao uwezo wa kujadiliana bei ya mazao na wanunuzi na hata kupanga mikataba ya mauzo kisheria. Aidha uwezo wa kuhifadhi mazao ghalani unasaidia kupanga kuyauza kwa muda muafaka wakati mahitaji ya wanunuzi yanapokuwa juu. Wakati wa mavuno mara nyingi bei huwa ndogo. Hivyo wanachama watakuwa na fursa ya kuyauza mazao kwa bei ya juu wakati bei ya sokoni itakapopanda kutokana na upungufu wa mazao katika soko na hivyo mahitaji kuongezeka.
- Hayo ni baadhi tu ya manufaa ya vyama vya wakulima wadogo kuungana katika mashirikisho. Wahariri wa MTAFUTAJI wanapenda kuwapongeza sana wakulima wa Morogoro kwa kuunda shirikisho. Wanatoa ushauri wa kulisajili shirikisho hilo haraka iwapo halijasajiliwa, ili manufaa yake yaonekane na liwe la kupigiwa mfano ambao utaigwa na wengine.

Mtafutaji mag2.indd 20 6/28/05 2:44:37 PM

MASHARTI YA MIKOPO YAWAATHIRI WAKULIMA WADOGO WA MIWA

Merina Robert, Morogoro

Kutokuwa na dhamana katika mabenki kumewacheleweshea mikopo wakulima wa miwa hali ambayo imesababisha kuchelewa kuanza kwa msimu wa kilimo mwaka huu na wakulima kupata mazao duni.

Hayo yalisemwa na wakulima wa vyama vya wakulima wa miwa wa nje wa Mtibwa (MOA), Ruhembe(ROA) na Kilombero(KSGA) wakati wa mkutano wa kubuni mipango baina ya mradi wa DAI PESA na Chama cha Wakulima wa Miwa Tanzania(TASGA) uliofanyika mapema mwaka huu kwenye hoteli ya Oasis mjini hapa. Kwa mujibu wa maelezo ya wakulima hao taasisi zinazotoa mikopo huchelewa kuwapatia mikopo, kwani taasisi hizo zinapaswa kuchunguza kwa umakini zaidi ili kubaini kama kweli waombaji ni wakulima wa zao hilo na wanastahili kukopeshwa. "Utakuta wakati wa msimu wa kilimo umefika, lakini mkulima bado hajapatiwa mkopo na anapopatiwa mkopo muda wa msimu wa kilimo unakaribia kuisha," walisema wakulima hao.

Wakulima hao walisema pia kwamba wanakabiliwa na tatizo la mkataba wa mauzo kati yao na manejimenti za viwanda vinavyonunua zao hilo. Kwa takriban miaka minne bado suala hilo halijapatiwa ufumbuzi. Hali hiyo inasababisha wakulima kupewa bei ndogo isiyolingana na jasho lao wanalovuja katika uzalishaji. Kama vile hilo ni dogo, kila kiwanda hutoa bei yake chenyewe, jambo ambalo linawavunja moyo wakulima hao; hususan wale wa Mtibwa, ambao hulipwa kiwango kidogo sana.

CHAMA CHA USHIRIKA KUANZISHA SEKONDARI

Na Albano Midelo, Songea

Chama cha Ushirika cha Wilaya za Songea na Namtumbo (SONAMCU) mwaka huu kinatarajia kuanzisha shule sekondari ya ushirika itakayokuwa na kidato cha kwanza hadi cha sita. Hayo yalisemwa na Meneja wa SONAMCU Bwana SALUM MBUYU alipoongea na jarida hili ofisini kwake mjini hapa hivi karibuni.

Bwana Mbuyu alifafanua kwamba SONAMCU ilichukua uamuzi huo ili kuwawezesha wanafunzi wanaotoka katika vyama vya ushirika vya Msingi zaidi ya 43 katika Wilaya za Songea na Namtumbo kupata nafasi za masomo ya sekondari. Alieleza kwamba uongozi wa SONAMCU ulikuwa umekwisha kuwasiliana na Serikali kuhusu kuchagua eneo moja kati ya maeneo matatu yaliyopendekezwa kwa ajili ya ujenzi wa sekondari hiyo.

Wakati huo huo SONAMCU mwaka huu inatarajia kuiboresha Hoteli yake ya ANGONI ARMS iliyopo



Mtafutaji mag2.indd 21 6/28/05 2:44:40 PM

maeneo ya Mahenge Mjini hapa, ili iwe na hadhi ya kitalii.
Kwa mujibu wa maelezo ya Bwana Mbuyu ujenzi wa ukumbi wa burudani katika eneo la chini ya ardhi ili kuzuia kelele kwa wageni, bwawa la kuogelea pamoja na eneo la michezo ya watoto unatarajia kufanyika mwaka huu.

Akizungumzia baadhi ya mafanikio ya chama hicho cha Ushirika, meneja huyo alisema kwamba SONAMCU imeweza kutoa elimu ya kuboresha uzalishaji wa zao la tumbaku na sasa zaidi ya asilimia 75 hadi 80 ya tumbaku inayozalishwa inakuwa katika madaraja ya kwanza, pili na tatu.

Kuhusu matatizo, Bw.Mbuya alisema kwamba SONAMCU inakabiliwa na tatizo la wakulima kushindwa kulipa mikopo ya pembejeo, hasa unapotokea ukame na wakulima kufia kwenye matembe ya tumbaku kwa bahati mbaya.

SOMO LA BIASHARA NA FAMILIA

Na Kundaeli E. Kawa, OIC Tanzania

LENGO:Kuwawezesha wafanyabiashara kutenganisha mahitaji ya biashara na yale ya familia.

Mafunzo haya yamegawanyika katika sehemu tatu.

1.Biashara na mwenye biashara: Somo hili linahusu kwanza mahitaji ya biashara na ya pili ni mahitaji ya familia. Ni muhimu kuzitenganisha fedha za biashara na zile za familia kwa kuwa na akaunti mbili tofauti; moja kwa ajili ya matumizi ya biashara na nyingine kwa ajili ya matumizi ya familia.

2. Biashara na Mazingira yanayoizunguka
Somo hili linahusu tatizo la wanafamilia na marafiki wanavyoweza kuiingilia na kuiathiri biashara yako kwa kutokuwa tayari kulipia bidhaa au huduma walizopewa, au kwa kuchukua au kukopa fedha taslimu toka kwenye biashara. Somo linaeleza njia mbali mbali za kuyepuka matatizo hayo, pamoja na kutoa hadhari juu ya kukopesha, kuwaelimisha wateja na umma.

3. Biashara na Wadau mbali mbali.
Wadau muhimu wa biashara yako ni pamoja na wagavi, wateja, wafanyakazi, mabeki, na serikali. Somo hili linaonyesha mahusiano na kutegemeana katika kuchangia kukuza uchumi wa taifa kati ya mfanyabiashara na wadau wengine. Iwapo mdau mmoja atakuwa dhaifu au hawajibiki ipasavyo basi mfumo mzima unaathirika. Kwa mfano iwapo mgavi haleti mali ghafi kwa wakati, au mteja halipii bidhaa alizokopa, mfanya biashara halipi kodi, au benki haiko tayari kuwapa mikopo mfanyabiashara, au mfanyakazi ni mbadhilifu mfumo mzima wa biashara utakwama na maendeleo yataathirika vibaya.

HITIMISHO:

Mfanyabiashara anashauriwa kuzingatia yafuatayo:

- Wafanyabiashara wengi hupata hasara na biashara zao hufa kwa sababu hawatenganishi pesa za familia na pesa za biashara. Pesa za biashara zitumike kuikuza biashara na pesa za matumizi ya familia ni zile za mshahara ambao mmililki wa biashara hujilipa kwa mwezi kutokana na biashara yake.

- Biashara ni kazi ambayo ni lazima itengeneze faida na mshahara wa mwenye biashara ambao ndio malipo ya nguvu yake. Hivyo inashauriwa kwamba biashara yoyote ni lazima itengeneze pesa za kujiendesha yenyewe na ile ya kumlipa mmililki, yaani mshahara wa mfanyabiashara kwa mwezi.

- Familia haitakiwi kutumia pesa za biashara kwa ajili ya kugharamia mambo ya kifamilia, kwa mfano matibabu, chakula, elimu au michango ya sherehe mbalimbali, bali mshahara anaojilipia mfanyabiashara kutokana biashara ndio utumike.

Mtafutaji mag2.indd 22 6/28/05 2:44:43 PM

MJUE "RAH P", MSICHANA ANAYEJITAFUTIA RIZIKI KWA MUZIKI

Na Nicco Gilliard

KATIKA safu hii ya aina yake katika jarida hili kwa mara ya kwanza tunachambua jinsi msanii ambaye bado ni msichana anavyojaribu kupambana na maisha au kujitafutia riziki kwa njia ya muziki. Huyu si mwingine bali ni "Rah P,". Nicco Gilliard anakuchambulia kwa undani zaidi.

Ni msanii mrembo vya kutosha na unaweza kushangaa ilikuwaje dada huyu akaamua kujiingiza kwenye fani hii ya wagumu...!!! Akiwa jukwaani mitindo yake ya kucheza ni ya kigumu ile mbaya na hata mavazi anayovaa ni ya kigumugumu... mikao yake ndiyo balaa zaidi na hii nadhani inatokana na kucheza muziki wa Hiphop.

Msanii anayezungumziwa hapa ni Fredinah Pey-ton ambaye hapa Der-Es-Salaam anajulikana sana kwa jina la Rah P, jina ambalo limetokana na herufi chache za jina lake.

Rah P alizaliwa mwaka 1986 mkoani Shinyanga akiwa mtoto wa pili kati ya watoto wanne wa mzee Peyton. Alipata elimu yake ya msingi nchini Kenya na alihitimu kidato cha nne huko Uganda, kabla ya kuendelea huko huko Uganda ambako hivi karibuni ameingia kidato cha tano.

Mwanadada huyu asiyekuwa na historia kubwa katika ulimwengu wa muziki anasema alianza kuimba baada ya kuwa mpenzi mkubwa wa wanamuziki kama akina Mc Lyte, Queen Pen na Destiny Child. Mara nyingi alikuwa anaigiza nyimbo za wanadada hao na kuzicheza kwenye maonyesho mbalimbali ya muziki kati ya shule mbalimbali. Jambo hili lilimwongezea umaarufu mkubwa huku mama yake mzazi akipinga vikali kitendo cha bintie kujishughulisha na muziki akiwa bado shuleni; lakini akiungwa mkono na dada yake mkubwa, Georgia.

Mwanzoni mwa mwaka 2003 nyota ya kuwa mwanamuziki ilianza kumng'aria Fredinah baada ya kupata nafasi ya kushiriki katika tamasha moja la muziki huko Butiama na Shinyanga huku kukiwa na wakali wengine, akina Mr Nice na Benjamin wa Mambo Jambo waliokuwa ziarani mkoani humo. Baada ya hapo ndipo mama yake alipoanza kumruhusu Fredinah kuwa mwanamuziki, ila kwa masharti ya kumaliza shule kwanza au kucheza muziki wakati wa likizo tu.

"Nilipomaliza kidato cha nne mwaka 2004 nikatia timu Dar es Salaam ambapo nilifanikiwa kurekodi "track" yangu ya kwanza niliyoipa jina la "HAYAKUHUSU" ndani ya studio za Bongo Records, chini ya mtengenezaji Pfunk a.k.a Majani,"
alisimulia Rah P.

Akielezea zaidi shughuli zake za kimuziki anasema hivi sasa anazifanya kwa taabu kidogo kwa sababu ya masomo, lakini kila likizo akija Dar anajitahidi kutengeneza kanda moja au mbili. Iwapo mambo yataenda kama yalivyopangwa basi anategemea mpaka mwezi Desemba mwaka huu atakuwa amemaliza albamu kali yenye kila kitu ambacho kinastahili kuwepo kwenye albamu ya mwanamuziki makini.

Akielezea jinsi alivyojizatiti kwenye ushindani wa kimuziki alisema.... "mi nitatoa nyimbo zenye ujumbe na flavour, japokuwa zitakuwa za aina ya wagumu zaidi na sina shaka zitakubaliwa vizuri kwani hata mwanzo wangu haukuwa mbaya. Nawashukuru sana wapenzi wa hiphop kwa kuipokea vizuri kazi yangu iliyopita," alimalizia Rah P.

Rah P anapenda kuwapa ujumbe wasanii wenzake wa kike kwamba waendelee kukomaa tu; wasikubali kuingia katika biashara nyingine au kukwamishwa kwa njia yoyote.

Mtafutaji mag2.indd 23 6/28/05 2:44:45 PM

TATIZO LA AJIRA KWA VIJANA

Na Elizabeth Ndetalao, Dar es Salaam

Ajira ni kazi yoyote halali awezayo kuifanya mtu yeyote, mwanaume au mwanamke na mahali popote ili kujipatia riziki. Ajira yaweza kuwa binafsi au ya kuajiriwa.

Vijana wengi wamekuwa wakikimbilia mijini toka vijijini, wakidhani kwamba huko watapata ajira. Wanasahau kwamba ajira yaweza kupatikana popote. Wafikapo mjini wanawakuta wenzao wengi hawana kazi. Hali hii inasababisha mlundikano wa vijana wengi wasio na ajira wasomi na wasioelimika, wakiwa na mawazo na matumaini ya kupata kazi ya kuajiriwa na si kujiajiri.

Baadhi ya sababu za ukosefu wa ajira:
Vijana wengi hawana sifa za kutosha za kuwawezesha kupata ajira, kwa mfano:-

(i) Elimu
Elimu inayotolewa shuleni haitoshi na hailingani na mazingira wanamoishi au waendayo kuishi vijana na kufanya kazi. Pia vijana hawapati elimu ya ubunifu wa kujiajiri kulingana na hali halisi ya maisha inavyobadilika. Vijana wengi bado wana mawazo ya kuajiriwa kwenye makampuni makubwa na maofisi ya serikali.

(ii) Uzoefu
Baadhi ya vijana hawana ujuzi wa kutosha na wale walio na ujuzi na elimu ya juu hawana uzoefu wa kazi. Wanakuwa wametoka tu shuleni na vyuoni. Waajiri wengi binafsi wanahitaji kuajiri wafanyakazi wenye uzoefu wa kazi husika.

Vijana kama hawa wanaweza kujiajiri na kujipatia kipato cha uhakika wakishauriwa

(iii) Malengo

Vijana wengi hawana malengo katika masomo yao. Wanasoma tu ili muradi wafike chuo kikuu, lakini hawajui baadaye watafanya nini na wapi.
Kwa mfano, kijana anaweza kusomea kozi yoyote pasipo kujua ajira zipo au la, akitegemea kwamba ataajiriwa na serikali, wakati serikali haiwezi kutoa ajira kwa watu wote. Ndiyo maana wasomi wengi wapo mitaani kwa sababu au hawataki au hawazijui fursa za kujiajiri.

(iv) Kutokujiamini

Vijana wengi hawajiamini kwamba wanaweza kufanya kazi au kuwa na ubunifu fulani wao wenyewe bila mfadhili. Wamebaki kuilaumu serikali tu.

Pia hawajui wafanye nini au waanzie wapi.
Ushauri: Elimu inayotolewa kwa vijana itoe mafunzo ya ubunifu wa kazi za kujiajiri k.m. mbinu za biashara na kilimo na vipengele vifuatavyo vipewe umuhimu:-

1. Vijana waeleweshwe kwamba mambo yamebadilika sasa na kwamba wanatakiwa

kuchangamka na kujiajiri, kwani wasomi nao ni wengi, na kuna ushindani toka nje ya nchi katika sera ya utandawazi

2. Vijana waelimishwe kwamba ajira ni popote, mjini au vijijini ili mradi inalipa.
3. Vijana wapewe elimu ya ubunifu wa kazi za kujiajiri kulingana na maeneo wanakoishi, na

4. Wafunzwe pia kuwa wajasiriamali, kwani baadhi yao wanaanza miradi lakini baadaye wanakata tamaa wakiona mapato hayatoshi. Waandaliwe kuwa "watafutaji" ili waache kukaa magengeni na kujiingiza katika vitendo viovu vya utumiaji wa mihadarati, ujambazi na ukahaba ambao utawaletea UKIMWI. Taifa litaangamia.

Mtafutaji mag2.indd 24 6/28/05 2:44:47 PM

OIC TANZANIA INATOA USHAURI NA MAFUNZO YAFUATAYO:

- Ujasiriamali
- Anzisha na Endeleza Biashara Yako
- Masoko, Upangaji Gharama na Bei
- Huduma kwa Mteja
- Uendeshaji wa Mikopo
- Uendeshaji wa Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali
- Tathmini na Ufuatiliaji wa Utekelezaji Miradi
- Mafunzo kwa wajumbe wa Bodi za Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali
- Mafunzo kwa ajili ya kuzifanya NGO ziwe endelevu
- Mafunzo ya Utengenezaji wa Batik, Tie and Dye
- Usindikaji wa Vyakula
- Mafunzo ya Stadi za Maisha

UFAFANUZI WA SHERIA YA UANDIKISHAJI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOs)

Na Abel Lyimo: Mshauri wa Vikundi na Sera katika mradi wa DAI PESA unaofadhiliwa naUSAID.

Kwenye toleo la kwanza la jarida hili la "Mtafutaji" niliandika makala iliyohusu uandikishaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) ambao unafanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kwa vile vikundi vingi vya wakulima vinavyosaidiwa na mradi wa DAI PESA vilikuwa kwenye hatua za uandikishaji, tulishauri vijaze fomu zilizotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais na vikundi vingi vilifanya hivyo. Nilipowasilisha baadhi ya fomu zilizojazwa na baadhi ya vikundi vya wakulima, ofisa wa Ofisi wa Makamu wa Rais, kitengo cha uandikishaji mashirika yasiyo ya serikali alizipitia na baada ya maswali kadhaa ilionekana kuwa ingawa vikundi hivyo si vya kiserikali, havina sifa ya kuitwa "NGOs" na hivyo akakataa kuendelea kuviandikisha.

Kufuatana na maelezo ya ofisa huyo, shirika lisilo la kiserikali ni lazima lilenge kutoa huduma zake kaika eneo kubwa kama wilaya, mkoa n.k. na kwa watu wote. Vikundi vingi vinavyosaidiwa na mradi wa DAI PESA vimelenga kutoa huduma kwa wanachama wao tu walio katika ngazi za vijiji, na mahali pengine vitongoji.

Shirika lisilo la kiserikali lazima liwe na ofisi na linatakiwa kuwa na wataalamu wa kutoa huduma zilizokusudiwa kwa watu wote wanaoishi katika eneo lililolengwa, na si kwa wanachama tu.

Kwa ufupi vikundi vinavyosaidiwa na mradi wa DAI PESA ni vidogo, dhaifu, havina wataalamu wala fedha na havina sifa za kuandikishwa kama mashirika yasiyo ya kiserikali chini ya mfumo mpya wa kuandikisha mashirika ya aina hiyo, yaani "NGO".

Wizara ya Mambo ya Ndani inaendelea kuandikisha vikundi au "Associations" kama ilivyokuwa awali. Kwa sababu hii tunashauri vikundi vinavyosaidiwa na mradi wa DAI PESA ambavyo havijaandikishwa viendelee kuandikishwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, kitengo cha kuandikisha vyama/vikundi ("Associations"). Waombaji wanatakiwa wajaze fomu mbili: SO1 na SO2 zinazotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Fomu hizo zinapatikana kwenye ofisi zote za mikoa na wilaya za mradi wa DAI PESA. Kila kikundi kinachoomba kusajiliwa kinatakiwa si tu kujaza fomu zilizotajwa hapo juu, bali pia kutayarisha kumbukumbu za kikao kilichopitisha maamuzi ya kukianzisha kikundi husika zikionyesha wanachama waanzilishi na sahihi zao. Aidha kikundi kinatakiwa kiambatanishe katiba, kumbukumbu za kikao kilichoipitisha katiba na barua ya kuomba kusajiliwa ambayo itatumwa pamoja na viambatanisho hivyo kwa msajili wa vyama, Wizara ya Mambo ya Ndani, kitengo cha kusajili vyama.

Pia vikundi vinatakiwa kupata barua ya Mkuu wa Wilaya yao ya kuvitambua vyama hivyo na vinatakiwa kuwakilisha ada zifuatazo:-

i) Kiingilio 10,000/=

Mtafutaji mag2.indd 25 6/28/05 2:44:51 PM

ii) Ada ya kila mwaka 40,000/=
iii) Ada ya kuandikishwa 100,000/=
Jumla 150,000/=

Kila mwaka vikundi vinatakiwa kulipa ada ya Tshs 40,000/= na vinatakiwa kutayarisha ripoti ya maendeleo, mapato na matumizi.

Vikundi vinavyosaidiwa na mradi wa DAI PESA vitasaidiwa na maofisa mradi walioko mikoani na wilayani kujaza fomu na kuelekezwa utaratibu mzima wa uandikishwaji.

Ikumbukwe kwamba vikundi/vyama ambavyo havijasajiliwa havina haki kisheria, haviwezi kusaini mikataba mbalimbali kisheria, haviwezi kukopa wala kukopeshwa kisheria, au kufungua akaunti benki na haviwezi kuwa viendelevu.

Tunavihimiza vikundi vyote ambavyo havijasajiliwa vijisajili mara moja. Mradi wa DAI PESA unasaidia kukusanya fomu zote, kuzipeleka kwenye ofisi husika, kufuatilia uandikishwaji na kupeleka vyeti vya usajili kwa vikundi vijijini.

Ni vema kuitumia fursa hii vizuri, kwani mradi utakapokoma vikundi vitaingia gharama kubwa sana kujisajili.

SHIRIKA LA PRIDE TANZANIA LAKOPESHA WAFANYAKAZI

NA Albano Midelo, Songea

Shirika lisilo la kiserikali la PRIDE TANZANIA tawi la Songea litatoa mikopo ya fedha kati ya shilingi laki mbili hadi milioni 15 kulingana na mshahara wa mfanyakazi, kuanzia miezi miwili ijayo. ''Hivi sasa tunasubiri sera na marekebisho ya mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu ili mikopo hiyo ianze kutolewa kwa wafanyakazi kwa masharti nafuu'', alisema Meneja wa shirika hilo, tawi la Songea, Bw.Victor Mhagama alipoongea na MTAFUTAJI ofisini kwake.

Akielezea maendeleo ya shirika hilo tawi la Songea, meneja huyo alisema kwamba jumla ya shilingi bilioni moja na milioni mia nne tisini na nne zilikopeshwa kwa wateja katika kipindi cha kuanzia mwaka 1998 hadi mwaka 2004, ambapo marejesho ya mikopo hiyo yalikuwa ni asilimia 100. Katika kipindi hicho wateja wa PRIDE TANZANIA Songea walijiwekea jumla ya akiba ya shilingi milioni 123.

Bwana Mhagama aliendelea kusema kwamba wateja wa shirika hilo waliongezeka kutoka wanachama 150 mwaka 1998 hadi wanachama 1412 mwaka 2004 na kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita shirika hilo limewakopesha wanachama wake 542 jumla ya shilingi milioni 269.

Shirika la Pride Tanzania lilifungua rasmi tawi la Songea mwaka 1998 na lina matawi 26 katika nchi nzima.

WAKULIMA WA MBOGAMBOGA WAHIMIZWA KUUNDA VIKUNDI

Merina Robert, Morogoro

Wakulima wameshauriwa kuunda vikundi ili waweze kujadili matatizo yao na kuyapatia ufumbuzi kwani mmoja mmoja hawataweza kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo.

Ushauri huo umetolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa mradi wa DAI PESA, Bw. Joseph Burke wakati wa ziara yake mkoani hapa alipotembelea vikundi vya wakulima wa mbogamboga na matunda vya Twighutze cha Nyandira katika tarafa ya Mgeta na kikundi cha wakulima kata ya Kikeo(CHAWAKAKI).

Bw.Burke alisema kwamba wakulima, hususan wa kata ya Kikeo wilayani Mvomero ambao wanakabiliwa na tatizo la usafiri, hawataweza kulitatua tatizo hilo mmoja mmoja bali kwa kupitia vikundi vya ushirika vya wakulima. Burke aliendelea kusema kwamba ushirika ni jambo la

Mtafutaji mag2.indd 26 6/28/05 2:44:53 PM

msingi katika kujenga mshikamano ulio sahihi wa wakulima ili wafanikiwe kuyatatua matatizo yanayowakabili katika maeneo husika. "Hata wafadhili hawawezi kuwasaidia bila kuwa katika vikundi vya ushirika vya wakulima, kwani ushirika ndio utakaowafanya muweze kutambulika kwa wafadhili", alisema Burke.

Katika ziara hiyo Bw. Burke aliongozana na Mratibu wa mradi wa DAI PESA, kanda namba moja ambayo inajumuisha mikoa ya Tanga na Morogoro, Bwana Canute Temu ambaye alishauri kwamba ili kuhakisha kwamba wanajikwamua kiuchumi ni vema wakulima walime kibiashara katika vikundi pamoja na kuwa na vyama vya kuweka na kukopa. Canute Temu aliendelea kueleza kwamba mradi wa DAI PESA unalenga kuwapatia mafunzo wakulima ili waweze kuendesha kilimo kibiashara na kuboresha uendeshaji wa vyama vya kuweka na kukopa(SACCOS) vilivyopo, pamoja na kuanzisha SACCOS mpya.

Wakulima wengi hususan wa kata ya Kikeo, walisema kwamba tangu nchi hii ipate uhuru hawajawahi kupewa mradi wowote wa kuwaelimisha juu ya kilimo bora pamoja na ufugaji, na kwamba hiyo ilikuwa fursa yao ya kwanza kupata wataalam ambao walitoka kwenye wa Mradi wa DAI PESA. Aidha waliomba wapewe elimu juu ya kilimo bora cha mboga mboga na matunda ili waweze kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao yao.

Wakilalamika kuhusu tatizo la ubovu wa barabara walisema kwamba wakati wa mvua magari hayafiki eneo la kata ya Kikeo.
Kutokana na tatizo hilo wanalazimika kubeba mazao kichwani na kutembea kwa masaa matano hadi kulifikia soko la wakulima la Nyandira na kutembea masaa hayo hayo wanaporudi kwenye maskani yao. Hali hii huwavunja moyo sana, kiasi kwamba nyakati nyingine wakulima wanaamua kuwauzia mazao yao walanguzi kwa bei ya kutupa.

Nao wakulima hao wa mboga mboga waliueleza ugeni huo kwamba tatizo lao kubwa ni ukosefu wa utaalam wa kutosha kutokana na maafisa ugani katika maeneo ya vijiji kutowajibika ipasavyo.

Zao la kabichi zinazolimwa Mgeta (Morogoro)

VIJUE VIKUNDI VYA AKINA MAMA WA TEMEKE VILIVYO KATIKA MRADI WA WEP

Na Halima Rashidi, Mratibu wa WEP/OIC TANZANIA

Katika toleo la kwanza tulitoa maelezo mafupi kuhusu mradi wa OIC Tanzania wa kuwaendeleza wanawake (yaani WEP). Tunaendelea kutoa maelezo ya vikundi mbalimbali ambavyo vinanufaika na huduma za mafunzo na mikopo toka WEP.

KIKUNDI CHA KITUNZE KIDUMU

Maskani ya kikundi hiki ni eneo la Keko Sadani wilayani Temeke. Kikundi hiki, kama vilivyo vingine katika mradi huu wa kuwapa wanawake uwezo wa kiuchumi (yaani WEP), ni cha wafanyabiashara ndogondogo. Akina mama kumi walijiunga mwaka 2003 ili waweze kupewa mikopo inayotolewa na WEP baada ya kupewa mafunzo ya ujasiriamali. Walikiita kikundi chao KITUNZE KIDUMU.
Akinamama hawa wanajishughulisha na ufugaji wa kuku na kilimo cha bustani za mbogamboga.

Vikundi vilivyo katika mradi wa WEP vinachagua uongozi kidemokrasia. Viongozi wa Kitunze Kidumu ni hawa:-

Mtafutaji mag2.indd 27 6/28/05 2:44:56 PM

1. Janet Mwita — Mwenyekiti
2. Stella Elias — Mweka Hazina
3. Yunis Elias — Katibu

Wanachama wa kikundi wanashiriki katika mipango na maamuzi yahusuyo biashara zao. Wanachama wa Kitunze Kidumu ni hawa:-

4. Gloria Chiposi
5. Jeni Zephania
6. Amina Zephania

Mfanyabiashara wa mbogamboga sokoni

7. Tumaini Mwamfupi
8. Maula Kastory
9. Rukia Hassani
10. Cecilia Ndanshau

Katika muda wa mwaka mmoja uliopita kikundi hiki kimepewa mkopo wa jumla ya shilingi milioni moja na laki tano (1,500,000) yaani mkopo wa kwanza wa sh. 500,000/= na wa pili sh 1,000,000. Marejesho ya kila fungu la mkopo hufanywa katika kipindi cha miezi sita. Walipotembelewa na Mratibu wa mradi wa WEP kama utaratibu wake wa kawaida, wanachama wa kikundi hiki walionyesha kufurahishwa na mkopo huo na walikiri kwamba umekuwa wa manufaa makubwa kwao.

Janeth Mwita, ambaye ni Mwenyekiti wa kikundi, alikuwa na haya ya kusema "Kabla ya kupata mkopo nilikuwa na matuta manne tu ya mchicha ambayo yalikuwa yananipa sh 24,000 kila msimu wa mavuno. Lakini baada ya kupata mkopo niliweza kuongezea matuta mengine matano, kuajiri kijana mmoja wa kunisaidia kumwagilia na kulima matuta ya mchicha, na niliweza kununua mbolea.
Mavuno yameongezeka na hivi sasa naweza kuuza tuta moja la mchicha kwa bei ya jumla ya shilingi elfu nane (8,000) na hivyo kuweza kupata sh elfu sabini na mbili kwa msimu. Naweza kuuza tuta kwa shilingi elfu nane kwani mchicha wangu sasa ni bora zaidi kutokana na kutumia mbolea".

Janet aliendela kuielezea furaha yake:
" Nawashukuru sana OICT, kwani sasa naweza kupata mapato ya kuridhisha kutokana na biashara yangu ya kilimo cha mboga na hivyo kuweza kumudu kuihudumia familia yangu vizuri zaidi nikilinganisha na hapo mwanzo.

Biashara hii imeniwezesha kulipa mkopo wangu bila matatizo kutokana na mafunzo ya biashara tuliyopata OICT na mauzo bora zaidi ya mboga. Naomba tuongezewe mkopo ili tuweze kuendelea kuboresha maisha yetu na ya familia na hivyo kuepukana na adui umaskini", aliongeza kusema Janet na bila kugugumiza akatoa ushauri ufuatao:-

"Pia nawashauri wanawake wenzangu kujiunga na vikundi ambavyo vina mtazamo wa kimaendeleo na hivyo kuweza kupata mitaji na kuendeleza au kuanzisha biashara mbalimbali".

Huu ni mfano mmoja tu wa jinsi wanawake wanavyoweza kujikomboa kutoka katika umaskini na kushiriki katika soko la ushindani. Akinamama, unganeni ili mpate uwezo wa kiuchumi na kuondokana na dhana ya kuwa magolikipa nyumbani.

Aidha, nikiongea kama Mratibu wa WEP, nawashauri wanavikundi mbali mbali waunganishe vikundi vyao katika mashirikisho. Hayo yatatuwezesha kuwa na sauti kubwa zaidi na kupewa mikopo kwa ajili ya miradi mikubwa zaidi, kwa mfano kilimo cha mashamba makubwa ya mbogamboga, maua, uvuvi, ufugaji na pia viwanda vya kusindika vyakula.

INAWEZEKANA, TUAMUE TU!

Mtafutaji mag2.indd 28 6/28/05 2:44:59 PM

SACCOS ZA WANAWAKE RUVUMA ZAKOPESHWA MIFUGO

Na Albano Midelo,

Ushirika wa Akiba na Mikopo wa Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma (ARUWOSAC) umetumia zaidi ya shilingi 47,000,000/= ili kutoa mikopo ya mifugo kwa SACCOS za wanawake katika wilaya zote Mkoani Ruvuma.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Msaidizi Mkoa wa ushirika huo Bibi GENIFRIDA HAULE, mifugo itakayotolewa ni ng'ombe wa maziwa 113 na mbuzi wa maziwa 100 ambao wanagharimu jumla ya shilingi milioni 47.

Alisema, kila Wilaya itapata ng'ombe wa maziwa 20 na mbuzi wa maziwa 20 isipokuwa Wilaya ya Songea Vijijini ambayo itapata ng'ombe wa maziwa 33 na mbuzi wa maziwa 20.

Bibi Haule alifafanua kwamba fedha hizo zimetolewa na Mfuko wa Nchi ya Japan kupitia Mbunge wa Viti Maalum Wanawake Mkoani hapa Mheshimiwa JENISTA MHAGAMA, ambaye ni mwanzilishi wa ARUWOSAC.

Bibi Haule alisisitiza kwamba mradi huo umeletwa mkoani hapa kwa ajili ya "kopa ng'ombe lipa ng'ombe na kopa mbuzi lipa mbuzi". Aidha alisema mradi huo umeingia katika SACCOS za wanawake kwa lengo la kuboresha afya za wanawake na watoto na kuongeza vipato vya familia kwa ujumla.

Katibu huyo aliongeza kwamba mradi huo utawawezesha wanawake kujijengea uwezo katika masuala ya ufugaji na tayari wanawake katika ushirika huo wamepata mafunzo ya ufugaji bora katika Chuo cha Mifugo Madaba, Wilayani Songea. Aidha alitoa wito kwa wanawake mkoani hapa kujiunga na SACCOS za wanawake ili kufikia lengo la Taifa la kuundoa umaskini ufikapo mwaka 2025.

Ushirika wa Akiba na Mikopo wa wanawake Mkoani hapa ulianzishwa rasmi mwaka 2002.

WADAU WATAKA MARUFUKU YA "LUMBESA" ITEKELEZWE.

Na Albano Midelo, Songea

Wadau wa kilimo Mkoani Ruvuma wameshauri kwamba sheria iliyopitishwa na Bunge mwezi Novemba mwaka jana ya kupiga marufuku mtindo wa baadhi ya wanunuzi wa mazao kujaza magunia kupita kiasi (yaani LUMBESA), itekelezwe haraka iwezekanavyo.

Wadau hao walitoa kauli hiyo hivi karibuni katika mkutano wao wa kwanza ulioandaliwa na Shirika la DAI PESA uliofanyika kwenye ukumbi wa DON BOSCO mjini hapa. Mkutano huo ulizungumzia jinsi vipimo visivyo halali (LUMBESA) vinavyoathiri maendeleo ya kilimo nchini.

Wadau hao waliyataja madhara ya "Lumbesa" kuwa ni pamoja na kumdhulumu mkulima mdogo kimapato, kumdhulumu msafirishaji, kuwaathiri vibaya kiafya wabeba mizigo (wapakizi), kuikosesha Serikali mapato na kuharibu takwimu sahihi za mazao.

Ili kukabiliana na tatizo la "Lumbesa" wadau hao wameshauri kwamba elimu kuhusu mizani halali itolewe kwa wadau wote wa kilimo kupitia vyombo vya habari, sanaa za maonyesho na mikutano ya hadhara. Aidha walishauri magulio na masoko yaimarishwe hadi vijijini ili mizani halali itumike wakati wa ununuzi wa mazao.

Walieleza kwamba kwa kuwa Serikali imepiga marufuku "lumbesa", ni vema utekelezaji wa sheria hiyo uanze haraka ili wakulima wasiendelee kukandamizwa na kunyonywa. Katika mkutano huo wadau hao walichagua kamati ya watu sita itakayokuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa sheria ya kufuta "lumbesa" Mkoani Ruvuma unaanza mara moja.

Wadau walioshiriki katika mkutano huo ni pamoja na wawakilishi wa Chama cha Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), Afisa Vipimo wa mkoa, wawakilishi wa Wakurugenzi wa Halmashauri zote Mkoani hapa, Wakala wa Barabara (TANROADS) na shirika linaloshughulikia maendeleo ya sekta binafsi la DAI PESA.

Mkutano wa pili utakaowakutanisha wadau hao kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria hiyo ulitarajiwa kufanyika mwezi Aprili mwaka huu.

Akifunga semina hiyo Mwenyekiti wa mafunzo hayo Bwana Vincent Mgimba alimhakikishia mwezeshaji kwamba elimu ambayo washiriki walipata itawafanya kuwa viongozi bora zaidi katika vikundi vyao.

Mtafutaji mag2.indd 29 6/28/05 2:45:02 PM

IRINGA VIJIJINI KUUAGA UMASKINI?

Na Mawazo Malembeka, Iringa.

Taarifa za uhakika zilizopatikana mjini Iringa hivi karibuni zinasema kwamba wakulima wa wilaya ya Iringa Vijijini sasa wanaweza kutajirika katika muda mfupi ujao, baada ya tatizo la ukosefu wa mitaji lililokuwa linawakabili kwa muda mrefu kupatiwa ufumbuzi. Imeelezwa kwamba neno ‘Umaskini’, likiwa na maana ya hali ya kushindwa kumudu maisha au mahitaji muhimu, sasa litakuwa historia katika wilaya hiyo.

Mkulima akiuza vitungu kando ya barabara

Neema zinaendelea kuwaangukia wakulima wadogo wa Iringa Vijijini. Neema ya kwanza ambayo wakulima hao wanayo ni kuwa chini ya Mradi wa DAI PESA, mradi ambao pamoja na mambo mengine unawafundisha kilimo cha kisasa na kutafuta masoko kwa pamoja, fursa ambayo awali hawakuwa nayo.

Katika siku za hivi karibuni, Mradi Shirikishi wa Mikopo na Akiba Vijijini (RPMS) umeanza kufanya kazi na wakulima hao, hususan walio katika mradi wa DAI PESA. Kwa mujibu wa Afisa Mtendaji wa RPMS, Bw.Henry Mwaijega, lengo la mradi huo ni kuwakopesha wakulima mitaji wakati wanapoihitaji.

“Bado hatujaanza rasmi kutoa mikopo lakini tanatarajia kuanza mapema iwezekanavyo na wakulima watakopeshwa kulingana na mahitaji ya kila mmoja, mkopo wa chini utakuwa Sh.150,000 na wa juu utakuwa Sh.300,000,” alisema Bw.Mwaijega.

Akizungumza kuhusu utaratibu wa mikopo Bw.Mwaijega alisema kwamba ili mkulima aweze kukopeshwa ni lazima awe mwanakikundi, awe na dhamana ya pesa taslimu asilimia 25 ya kiasi anachotaka kukopa, atoe ada ya uanachama ya Sh.2000 na awe na dhamana ya vitu vinavyohamishika kama samani, na kadhalika.

Afisa mtendaji huyo alifafanua kwamba riba ya mikopo hiyo itakuwa asilimia 2.5 na kwamba mkulima atarejesha mkopo katika kipindi cha miezi mitatu hadi minne, kulingana na zao analolima. “Sisi hatuwapangii muda wa kurejesha na wala muda wa kurejesha haukupangwa kulingana na kiasi cha pesa anachokopa mkulima, la hasha. Mkulima mwenyewe anapanga atarejesha mwezi gani kulingana na zao analolima (muda wa kuuza mazao yake),” alisisitiza Bw.Mwaijega.

Bw.Mwaijega aliongeza kwamba jumla ya mikopo 1703 yenye thamani ya Sh. milioni 102 ilitolewa mwaka jana na RPMS na lengo la mwaka huu ni kutoa mikopo 2,500 yenye thamani ya Sh.milioni 344.

Mradi wa RPMS ulianza mwaka 2000 lakini shughuli za kutoa mikopo zilianza rasmi mwaka juzi. Mradi huo unatekelezwa kwa majaribio katika wilaya za Iringa Vijijini na Kilolo kwenye kata nane za wilaya hizo, ambazo ni Mtitu, Dabaga, Ukumbi, Ilula, Magulilwa, Ifunda, Mgama na Ilole.

Mtafutaji mag2.indd 30 6/28/05 2:45:06 PM

RUVUMA WAFUNZWA KILIMO CHA PILIPILI MBOGA *(PAPRIKA)*

Na Albano Midelo, Songea

Viongozi 40 toka vikundi 19 vinavyolima pilipili mboga Mkoani Ruvuma walihudhuria mafunzo ya kilimo bora cha pilipili mboga yaliyoandaliwa na DAI PESA hivi karibuni. Mafunzo hayo ya siku nne yaliendeshwa katika ukumbi wa kituo cha DON BOSCO cha mjini hapa na yalihusu nadharia za hatua mbalimbali katika kilimo bora cha pilipili mboga. Hatua hizo ni pamoja na namna ya kutunza kitalu, upandaji wa miche, kuchagua miche, utunzaji wa shamba, uchumaji na ukaushaji wa zao hilo.

Mwezeshaji katika mafunzo hayo alikuwa Bwana CHEDI MHINA toka Kampuni ya Viungo Tanzania, (yaani "Tanzania Spices Limited") ya mjini Iringa, kampuni pekee inayonunua zao hilo. Bwana Chedi Mhina alimweleza mwandishi wa habari hizi matarajio yake makubwa kwamba kufuatia viongozi hao wa vikundi kupewa mafunzo, pilipili mboga zingezalishwa kwa ubora unaotakiwa. "Zao la paprika ni jipya mkoani Ruvuma. Hata hivyo, mafunzo niliyowapatia kwa siku nne yatawawezesha kuzalisha paprika yenye ubora zaidi", alisema.

Naye Afisa Mradi wa DAI PESA mkoani Ruvuma, Bwana Mays Mkwembe, aliwashauri washiriki hao kuzingatia mafunzo yaliyotolewa na mkufunzi huyo ili wakirudi makwao wawe walimu wazuri katika vikundi vyao.

Msimu huu wakulima 3000 katika wilaya za Songea na Namtumbo wamelima ekari 2264 za pilipili mboga na wanatarajia kupata jumla ya shilingi bilioni moja baada mauzo.

UZALISHAJI WA MIWA KUPANDA

Na Merina Robert, Morogoro

Uzalishaji wa miwa unatarajiwa kupanda toka tani 389,250 za sasa hadi kufikia tani 1,456,000 ifikapo mwaka 2010, kwa mujibu wa maelezo ya Katibu wa Chama cha Wakulima wa Miwa Tanzania yaani (TASGA), Bw. Sosthenes Magesse. Bw. Magesse alisema pia kwamba TSGA imesanifu mpango wake wa maendeleo wa miaka kumi ambao umejumuishwa katika mpango mkubwa wa maendeleo ya sekta ya sukari nchini.

Katibu huyo alitoa maelezo hayo wakati wa mkutano wa ushirikiano baina ya TSGA na mradi wa DAI PESA uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro na kuwashirikisha viongozi toka vyama vya wakulima wa miwa vya Mtibwa, Ruhembe na Kilombero.

Bw. Magesse aliongelea pia matarajio ya wanachama ya kuinua tija ya ardhi na kazi toka uzalishaji wa sasa wa tani 45 kwa hekta moja na kufikia tani 80 kwa hekta moja ifikapo mwaka 2010. Akiendelea kufafanua Bw. Magesse alisema kwamba awali, tangu kuanzishwa kwa makampuni ya Kilombero na Mtibwa mwaka 1960, wakulima wadogo wadogo wa miwa walitarajiwa kuzalisha viwango vidogo tu vya miwa, kama nyongeza juu ya uzalishaji wa mashamba ya kampuni hizo.

Akieleza kuhusu ukuaji wa uzalishaji wa miwa Bw. Magesse alisema kwamba kati ya mwaka 1991 na 2004/2005 mchango wa miwa ya wakulima wadogo wadogo umeongezeka toka asilimia 17% hadi 46% kwa upande wa Kilombero na toka asilimia 27% hadi asilimia 51% kwa Mtibwa, ya miwa yote inayosindikwa na viwanda hivyo. Mwenendo huu unaonyesha na kuthibitisha kuongezeka kwa umuhimu wa mchango wa wakulima wa miwa wadogo wadogo nchini. Alisema tangu mwaka 1998, viwanda hivyo vilipobinafsishwa, uzalishaji wa miwa wa wakulima wadogo wadogo katika kampuni ya Kilombero umeongezeka mara nne na katika kampuni ya Mtibwa umeongezeka maradufu.

Katika mkutano huo Bw. Magesse pia aliyapitia matatizo

Mtafutaji mag2.indd 31 6/28/05 2:45:09 PM

yanayowakabili wakulima wa miwa ambayo ni pamoja na mashamba kuathiriwa na mafuriko kutokana na kutokuwa na mifereji ya kuridhisha ya kuyaongoza na kuyatoa maji mashambani.

Matatizo mengine ni bei ndogo ya miwa wanayopewa wakulima, ugumu wa kupata fedha za mtaji za kuendeshea shughuli za kilimo,miundo mbinu duni,tija ndogo ya uzalishaji wa miwa kwa eneo,uhaba wa maafisa wataalamu, kodi kubwa ya zao la miwa, ucheleweshaji wa malipo kwa wakulima na ajali za moto kwa wakulima kuchomewa miwa yao.

Viongozi wa Shirikisho la Vikundi vya wakulima watembelea Moshi na Arusha

Na Abel Lyimo: Mshauri wa Vikundi na Sera katika mradi wa DAI PESA unaofadhiliwa naUSAID.

Viongozi wa vikundi vinavyosaidiwa na mradi wa DAI PESA ambavyo tayari vimeunda shirikisho hivi karibuni walivitembelea vikundi vya wakulima wa "kahawa spesheli" vya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Wakati wa ziara hiyo viongozi wa Shirikisho la Vikundi vya Wakulima wa Mpunga vya wilaya ya Mbarali, Vikundi vya MbogaMboga na Matunda vya mkoa wa Morogoro na Vikundi vya Machungwa vya mkoa wa Tanga, walivitembelea vikundi vya "kahawa spesheli" vya Mrimbouuwo,(Moshi vijijini), Amkeni (Moshi vijijini), Leguruki (Arumeru), Nombeko (Arumeru) na King'ori (Arumeru) ili kujionea shughuli za maendeleo zilizofanywa na vikundi hivyo. Viongozi hao pia walipata fursa ya kuhudhuria kikao cha menejimenti ya Shirikisho la Vikundi Vya Wakulima wa "Kahawa Spesheli" na kutembelea ofisi zao zilizoko Moshi mjini.

Kwa ufupi viongozi hao wa wakulima walijifunza mambo yafuatayo:

- Wingi wa wanachama si kigezo kikuu ili kikundi kiwe endelevu bali jambo muhimu ni kuwa na wanachama wenye moyo, upendo na ushirikiano.

- Vikundi vingi vya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha vilianza na wanachama wachache, saba hadi hamsini. Vikundi vingi bado vina wanachama wachache, lakini vinatoa huduma hata kwa wasio wanachama na vimepiga hatua kubwa sana.

- Kila kikundi kina ofisi na kimeajiri meneja ambaye anasimamia shughuli zote za maendeleo ya kikundi. Ili kikundi kiendelee ni lazima kiwe na wafanyakazi, hasa meneja ambao watabuni mbinu mbalimbali za kuongeza kipato cha wanachama.
- Serikali au mashirika ya umma yanapenda kuvisaidia vikundi ambavyo tayari vimeanza kuonyesha dalili ya kujitegemea. Kikundi cha Mrimbouuwo kilipata msaada wa shilingi milioni kumi na saba toka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa ajili ya kukiimarisha kiwanda chao cha kukoboa kahawa pamoja na kununua mashine mpya. Kikundi cha Amkeni kilipata msaada wa shilingi milioni kumi toka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa ajili ya kukarabati ofisi zao na kununua mashine mpya.

- Ili vikundi viendelee na viwe endelevu ni lazima viuze kwa pamoja mazao ya wanachama wao.
- Wanachama lazima wawe tayari kugharamia shughuli za maendeleo ya kikundi chao. Michango ni muhimu kwenye maendeleo ya kikundi.
- Viongozi lazima wawe wabunifu na wasijiingize kwenye siasa wala dini.
- Shirikisho ni muhimu sana hasa katika masuala ya masoko, ufanisi katika masoko ya nje, mawasiliano na mabenki, upatikanaji wa pembejeo n.k. kwani linaajiri waataalamu wenye uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali.

Baada ya ziara hiyo viongozi walipata ari ya mageuzi na wamepanga kuzungumza na wanachama wote wa vikundi vyao ili kuwaeleza waliyoyaona kwenye ziara hiyo na kujaribu kubuni mipango ya kutatua kero za wanachama.

RUMACU SACCOS YAJENGEWA UWEZO

Na Albano Midelo, Songea

Mfuko wa kukopesha Vyama vya Kuweka na Kukopa (yaani CFP) umekipa mkopo wa jumla ya shilingi milioni 28 Chama cha RUMACU SACCOS cha Mjini hapa, ili kukijengea uwezo wa kuwakopesha wanachama wake.

Akisoma taarifa kwenye Mkutano Mkuu wa Chama hicho uliofanyika tarehe 20/3/2005 kwenye Ukumbi wa Chuo cha Ushirika Songea, Katibu wa RUMACU SACCOS Bwana PAUL LWANDA alieleza kuwa fedha hizo zilitolewa kwa

Mtafutaji mag2.indd 32 6/28/05 2:45:13 PM

awamu tatu tofauti katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Bwana Lwanda alifafanua kwamba katika awamu ya kwanza CFP walitoa mkopo wa shilingi milioni nne, awamu ya pili shilingi milioni tisa na awamu ya tatu shilingi milioni 15.
Kwa upande wake, kamati ya mikopo ya RUMACU SACCOS iliidhinisha mikopo ya jumla ya shilingi zaidi ya milioni 18 kwa wanachama wake katika kipindi hicho. Bwana Lwanda aliendelea kueleza ya kuwa mapato ya SACCOS hiyo katika kipindi hicho yalifikia shilingi milioni 2.6, ambapo matumizi yalikuwa shilingi milioni 1.9 na faida ilikuwa shilingi zaidi ya laki sita. Aidha katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2004 HISA za wanachama zilikuwa na thamani ya shilingi milioni 1.4.

Akiuelezea mwelekeo na mtazamo wa RUMACU SACCOS kwa mwaka huu, Lwanda alisema kwamba chama hicho kinatarajia kuwawezesha wanachama wake kuanzisha miradi mbalimbali ili kuwainua kiuchumi.
RUMACU SACCOS inatarajia pia kuanzisha mradi wa usafiri wa mabasi madogo (yaani mini-buses) ambao unatafutiwa wabia nje ya nchi wanaoshughulika na miradi ya aina hiyo.

RUMACCU SACCOS ambayo ilianzishwa mwaka 1991 na hadi sasa ina wanachama 44, inakabiliwa na tatizo la wanachama kukiuka utaratibu wa marejesho ya mikopo, ambalo hatua madhubuti za kulidhibiti zimeandaliwa tayari.

WASHAURIWA KUTAFUTA MASOKO KUPITIA MITANDAO YA KOMPYUTA

Na Albano Midelo,Songea

Viongozi wa vikundi vya wakulima wa zao la pilipili mboga (paprika) toka wilaya za Songea na Namtumbo wameshauriwa kutafuta masoko ya zao hilo nje ya nchi kupitia mitandao ya kompyuta, badala ya kutegemea soko la ndani pekee.

Ushauri huo ulitolewa hivi karibuni na Bwana Rwelengera Mugyabuso toka Dar es Salaam alipokuwa anaendesha semina ya viongozi zaidi ya 100 wa vikundi na vijiji kwenye ukumbi wa Don Bosco mjini hapa iliyoandaliwa na DAI PESA. Aidha Bwana Mugyabuso aliwasisitizia viongozi hao kushirikiana na wakulima wa pilipili mboga katika kutafuta masoko na kwenda na wakati na dunia ya utandawazi.
Akizungumza kuhusu sifa za uongozi, Bwana Mugyabuso alieleza kwamba uongozi hauna maana ya kuwapigia watu kelele bali ni kuzungumza, kujadiliana na kutoa ushauri unaojenga. Akiiendeleza mada yake mwezeshaji huyo alifafanua kwamba inampasa kiogozi kutumia mifumo mbalimbali ya mawasiliano katika kukusanya na kusambaza habari kwa jamii inayomzunguka, na kwa hivyo hana budi kuwa na mahusiano mazuri na vyombo vya habari pamoja na asasi nyingine.

Katika semina hiyo viongozi hao walijifunza jinsi ya kuendesha vikao, mbinu za ushirikishaji na stadi za mawasiliano na mahusiano.

Naye Afisa Mradi wa DAI PESA Mkoani Ruvuma, Bwana MAYS MKWEMBE aliwaeleza viongozi hao kuwa lengo la DAI PESA ni kuwajenga wakulima wadogo kiuongozi ili waweze kuvisimamia ipasavyo vikundi wanavyoviongoza katika kilimo cha pilipili mboga kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa zao hilo na kuuondoa umaskini.

Alieleza zaidi kwamba hadi sasa DAI PESA imeanzisha miradi ya kilimo katika mikoa sita hapa nchini. Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Iringa (pilipili mboga na vitunguu), Morogoro (matunda na mbogamboga), Rukwa (alizeti), Ruvuma (pilipili mboga) na Mbeya (mpunga).

Mtafutaji mag2.indd 33 6/28/05 2:45:16 PM

Teknolojia yetu itumike kupambana na Umaskini

Na Fatma Msheri na Waeli John OICT

Teknolojia iliyo bora inasaidia sana katika kuharakisha maendeleo ya binadamu, kama vile kutumia mashine za kilimo badala ya jembe la mkono au mnyama, utengenezaji na hifadhi ya vyakula kwa usalama zaidi, uzalishaji wa nishati, bidhaa n.k. Aidha, kwa kutumia teknolojia bora vifaa vingine vinaweza kutengenezwa na kuuzwa katika soko la dunia kwa faida. Matumizi ya teknolojia bora husaidia pia katika kuhifadhi maliasili na mazingira kwa ujumla.

Tanzania ni mojawapo ya nchi maskini zaidi duniani na iko nyuma katika nyanja nyingi, ikiwemo ile ya teknolojia. Suala la kujiuliza ni kwa jinsi gani Tanzania inaweza kujikwamua kutoka kwenye umaskini wa kiteknolojia? Njia mojawapo ni ile ya kutumia teknolojia kutoka nchi zilizoendelea. Hatua hii inaweza kusaidia sana katika kupambana na umaskini. Kwa kutumia vifaa kama majiko ya umeme kutoka nchi zilozoendelea, kwa mfano, tunaweza kupunguza ukataji wa miti itumikayo kutengenezea mkaa kama nishati ya kupikia, na hivyo tutaweza kutunza mazingira yetu na kuyatumia vizuri zaidi kwa ajili ya maendeleo yetu na ya vizazi vijavyo. Tunaweza pia kutumia vifaa kama kompyuta ili kurahisisha mawasiliano, utendaji wa kazi na hifadhi ya kumbukumbu.

Hata hivyo, inatupasa tujiulize iwapo teknolojia ya wenzetu walioendelea kweli itawasaidia Watanzania wote? Maana tunapoongelea maendeleo hatuna budi kujumuisha wananchi wote. Teknolojia hiyo inahitaji kugharamiwa kwa kuinunua, kuitunza, na kuiendeleza. Hata ikitoholewa, je maskini wataimudu? Jibu lipo wazi, nalo ni HAPANA, hawataimudu.

Basi kuna umuhimu wa kuangalia jinsi gani tuitumie na tuiendeleze teknolojia yetu wenyewe ili kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Teknolojia yetu inaweza kutumika katika mazingira yetu na gharama zake ni nafuu ambazo hata mtu wa kipato cha chini anaweza kuzilipa.

Tunayo mifano mingi ya matumizi ya teknolojia yetu ambayo ikiboreshwa ni mkombozi mkubwa. Watu wengi wanatumia majiko ya mkaa yaliyotengenezwa hapa hapa nchini. Teknolojia hiyo imeboreshwa kiasi cha kutengeneza majiko yanayotumia mkaa kidogo sana kwa kupikia vyakula vingi jambo ambalo linasaidia sana kupunguza kasi ya ukataji miti, na hivyo husaidia kutunza mazingira. Majiko hayo yanahitaji kuboreshwa zaidi na zaidi, ili tuweze hata kukamata sehemu kubwa ya soko la nje ya nchi na wananchi kujipatia kipato kwa ajili ya maendeleo yao.

Siku za nyuma stadi ya usukaji ilitumika kutengeneza mikeka na majamvi. Lakini siku hizi hata mikoba inayotumiwa na akina mama inatengenezwa kwa kusukwa na inawavutia sana watalii. Hivyo usukaji unaweza kutuingizia fedha za kigeni, tukitafuta soko kubwa zaidi huko huko watokako watalii hao, licha ya kutosheleza mahitaji ya ndani. Kipato cha mafundi stadi wa usukaji, hasa wawe vijijini, kitakua na wataweza kumudu huduma zao za kila siku.

Stadi ya ufinyanzi nayo ikiendelezwa inaweza kutupatia mbadala mzuri wa vifaa vya kutoka nje ya nchi. Vyungu hutumiwa sana katika maeneo ya vijijini kwa ajili ya kupikia na hivyo hivyo wafinyanzi hutengeneza vyungu kwa ajili hiyo tu. Hali hii inasababisha soko lao kuwa dogo na lisilo na uhakika, kwani vyungu wavitengenezavyo ni vichache na havijulikani kwa wengi. Teknolojia hiyo inaweza kupanuliwa na kutumiwa kwa kutengeneza vyungu vya kupandia na kutunzia maua ambavyo hupendwa sana mijini na hata nchi za nje. Wafinyanzi wa vijijini wawezeshwe ili hali zao za maisha ziweze kuwa bora zaidi kwa kufinyanga vyungu vya kibiashara.

Teknolojia bora na rahisi ya kutengeneza nishati ya umeme kwa kutumia vinyesi vya wanyama na vitu vingine vya uoto itarahisisha upatikanaji wa nishati hiyo hata vijijini. Na hii ni teknolojia ambayo wananchi wa kawaida wanaweza kuitengeneza vizuri zaidi wakiungana katika vikundi. Umeme huo, na hata gesi ya kupikia kama itumiwayo kwenye kituo cha masista Wakatoliki pale Hombolo, Dodoma inaweza pia kutumika katika kutengeneza vifaa mbali mbali, kama vyungu, ufuaji wa visu na mapanga, kupikia vyakula, n.k. Mifano ya teknolojia yetu ipo mingi sana.

Basi, ili mradi teknolojia asilia inaweza kutumika katika kutengeneza mali bora na kurahisisha maisha ya mwananchi, kumwondoa kwenye hali duni na kumleta ndani ya mwelekeo tawala, serikali ishirikiane na wananchi katika kuiendeleza. Huu ni wakati ambapo tunashuhudia dunia yetu ikiwa kama "kijiji kimoja" kutokana na mfumo mpya wa kiuchumi ujulikanao kama utandawazi au kwa lugha ya kigeni "Globalization". Katika utandawazi huo nchi zote za ulimwengu zina fursa zaidi ya kushirikiana katika nyanja mbali mbali, ikiwemo biashara. Hata hivyo nchi hizi ambazo ni "kijiji kimoja" zinatofautiana sana kiteknolojia, kiuchumi na kwa mambo mengi mengine. Pengo kati ya nchi zilizoendelea na zile maskini linajidhihirisha wazi zaidi, na



Mtafutaji mag2.indd 34 6/28/05 2:45:18 PM

kwa juu juu inaonekana kwamba nchi zenye uchumi duni zinazidi kudidimia kimaendeleo, hasa kwa kuangalia hali za maisha ya wananchi wa kawaida. Tatizo kubwa ni uduni wa teknolojia za nchi zinazoendelea na uwezo mdogo wa kuzimudu teknolojia za nchi zilizoendelea. Hivyo ni muhimu kwa nchi maskini kuziendeleza teknolojia zao asilia.

Teknolojia bora na rahisi ya kutengeneza nishati ya umeme kwa kutumia vinyesi vya wanyama na vitu vingine vya uoto itarahisisha upatikanaji wa nishati hiyo hata vijijini. Na hii ni teknolojia ambayo wananchi wa kawaida wanaweza kuitengeneza vizuri zaidi wakiungana katika vikundi.

Umeme huo, na hata gesi ya kupikia kama itumiwayo kwenye kituo cha masista Wakatoliki pale Hombolo, Dodoma inaweza pia kutumika katika kutengeneza vifaa mbali mbali, kama vyungu, ufuaji wa visu na mapanga, kupikia vyakula, n.k. Mifano ya teknolojia yetu ipo mingi sana.
Basi, ili mradi teknolojia asilia inaweza kutumika katika kutengeneza mali bora na kurahisisha maisha ya mwananchi, kumwondoa kwenye hali duni na kumleta ndani ya mwelekeo tawala, serikali ishirikiane na wananchi katika kuiendeleza.

Utafiti wa mazingira

Utafiti wa mazingira kabla ya utekelezaji wa miradi mikubwa ni muhimu sana. Matokeo ya utafiti yataelekeza jinsi ya kuchukua hadhari juu ya athari zinazoweza kujitokeza, hususan katika miradi inayohusisha matumizi ya maliasili kama vile maziwa, mito, bahari misitu/miti n.k.

Pia ni muhimu kuyatumia matokeo ya utafiti wowote unaofanyika, na wenye miradi wawaelimisha wakazi wa maeneo iliko miradi yao ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuyazuia madhara yanayoweza kutokea na kubuni mbinu mbadala za kuyatunza mazingira yao.

Mfano mzuri wa wananchi wanavyotunza mazingira yao ni Mkoa wa Pwani. Mkoa huo unatoa kipaumbele kwa suala la utunzaji wa maliasili zilizopo baharini, kwani sehemu kubwa ya mkoa huo imezungukwa na Bahari ya Hindi. Pamoja na kutoa kipaumbele kwa raslimali za baharini Mkoa wa Pwani pia unaendesha miradi mingine kadhaa ya kuhifadhi mazingira, kwa mfano mradi wa utafiti wa mazingira ujulikanao kama "Rujiji Environmental Management Project-REMP" ambao unahusisha vijiji vinne vilivyopo kando kando ya mto Rufiji. Katika mradi huo ambao ulianzishwa mwaka 1998 vijiji hivyo vinapata msaada wa kiufundi toka shirika la kuhifadhi mazingira la kimataifa (IUCN) ambalo hivi karibuni lilishinda tunzo ya dola za Kimarekani milioni 30.

Kuhusu utunzajia wa misitu, wananchi hawakatazwi kujipatia riziki zitokanazo na misitu, bali kinachozuiwa ni ukataji miti ovyo ambao matokeo yake ni kutoweka kabisa hifadhi za misitu na viumbe hai vinavyoitegemea miti, yaani wanyama, wadudu na ndege. Sio hao tu hata maisha ya mwanadamu mweyewe yataathirika sana kwa kukosa mbao, mvua na vyanzo vya maji baada ya kuifyeka misitu. Ukosefu huo utadhoofisha nguvu zote za kuleta maendeleo.
Kwa makusudi kabisa serikali ya Tanzania inahimiza uwekezaji katika miradi mbalimbali ili kuharakisha uondoaji wa umaskini katika jamii. Hata hivyo miradi hiyo ambayo inatakiwa ilenge kuwakwamua wananchi kutoka katika lindi la umaskini haitakuwa na faida iwapo wawekezaji hawatafanya utafiti ili kuangalia jinsi ya kuzuia athari za kimazingira.

Hivi haya ni mazingira salama kwa binadamu ?

Mtafutaji mag2.indd 35 6/28/05 2:45:22 PM

NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

SOCIAL HEALTH INSURANCE SCHEME AT "NO EXTRA COST"

- Quality healthcare services for all employees and their dependants and the same amount of your monthly contribution.
- Outpatient services from curative care to specialized x-rays procedures including Dental, Optical.
- Inpatient services from basic investigations to major operation, referral to specialized hospitals.

High quality cost effective healthcare services provided all over Tanzania in medical care services and accredited private and public hospitals.

WE BUILD YOUR FUTURE